ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	-	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	-	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	-	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Tatu – Tarehe 25 Machi, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa idhini yako nawasilisha Hati Mezani ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula Nam. 3 ya Mwaka 1988 na Kutunga Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana
Hayo.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara juu ya Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 83

Kuinua Ufanisi wa Baraza la Wawakilishi

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza**:-**

Nchi ya Zanzibar ikiwa ni nchi ya pili inayounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaongozwa na Mamlaka tatu za Dola. Baraza la Wawakilishi, likiwa ni miongoni mwa Mamlaka hizo, ndio pekee lenye jukumu la kuisimamia Serikali na kuwafikia wananchi kwa urahisi iwapo waandishi wa habari watawezeshwa kutoa taarifa za Baraza kwa kufuata maadili ya kazi zao.

(a) Je, ni mara ngapi katika historia ya Zanzibar, Serikali imewajibika kwa Baraza la Wawakilishi pale inapotokezea haja hiyo.

(b) Mbali na utaratibu wa Kikatiba wa Rais kulihutubia Baraza. Kwa kuwa Rais ni sehemu ya Baraza la Wawakilishi. Je, anaweza kukutana na Wawakilishi kwa lengo la kubadilishana mawazo angalau kwa kuanzia na Wenyeviti na Makamo Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza.

(c) Kwa kuwa Baraza linaheshimu umuhimu na uhuru wa vyombo vya habari kutoa taarifa za Baraza, kuna sababu zipi zinazozuia waandishi hawa kupewa posho na malipo mengine yanayostahiki pale wanapofanya kazi zao kupitia vikao vya Baraza na Kamati za Kudumu.

(d) Ni lini Baraza la Wawakilishi litavitumia vyombo vya habari (Redio na Televisheni) kurusha moja kwa moja (*live*) Vikao vya Baraza na mijadala mbali mbali, badala ya utaratibu wa sasa wa kurusha vipindi vya masuala tu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwanza naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Hija kwa swali lake hili ambalo linadhirisha wazi uelewa mpana alionao Mhe. Mjumbe katika majukumu na wajibu wa Baraza la Wawakilishi kwa niaba ya wananchi katika kusimamia serikali na kuonesha umuhimu na mchango wa vyombo vya habari katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo naomba sasa kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Historia ya Zanzibar inaonyesha na kudhihirisha kwamba siku zote na mara zote Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikiwajibika ipasavyo kwa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa matakwa ya Katiba. Ndio maana Baraza la Wawakilishi limeweza kutekeleza majukumu yake Kikatiba ikiwemo kutunga sheria, kujadili shughuli za kila Wizara wakati wa Vikao vya Bajeti, kuuliza maswali mbali mbali kwa seriakli na kuidhinisha na kusimamia mipango ya mendeleo ya serikali. Kutokana na Baraza kutimiza majukumu hayo imewezesha demokrasia kuimarika zaidi nchini pamoja na kutoa nafasi ya kuwawakilisha vizuri wananchi katika chombo chao.

(b) Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni Rais wa watu na amechaguliwa na watu. Kwa hivyo, mbali na utaratibu wa

kikatiba wa Mheshimiwa Rais kulihutubia Baraza, Mheshimiwa Rais anaweza kukutana na Waheshimiwa Wawakilishi kwa lengo la kubadilishana mawazo sio tu na Wenyeviti na Makamo Wenyeviti wa Kamati tu bali na Wawakilishi wote na Wananchi kwa ujumla. Hata hivyo, Mhe. Rais tayari ametuarifu nia yake ya kutaka kukutana na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa nia ya kubadilishana mawazo.

(c) Napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mjumbe kwamba Baraza la Wawakilishi linaheshimu umuhimu wa uhuru wa Vyombo vya habari katika kutoa taarifa zinazohusu shughuli za Baraza. Baraza la Wawakilishi linaheshimu uhuru huo wa vyombo vya habari kwani Katiba ya Zanzibar ya 1984 kifungu cha 18 kimetoa uhuru wa kutafuta, kupokea na kutoa habari. Hata hivyo, jukumu la kuwalipa waandishi wa habari ni la taasisi husika ya habari ambayo mwandishi wa habari ameajiriwa kuifanyia kazi.

(d) Baraza la Wawakilishi linavikaribisha vyombo vyote vya habari ambavyo vina uwezo na vingependa kurusha matangazo ya shughuli za Baraza moja kwa moja (*live*) kufanya hivyo kwani itasaidia kufikisha taarifa halisi za Baraza la Wawakilishi kwa wananchi wote.

Naomba nichukue fursa hii kwamba wale wote wambao wapo tayari kurusha matangazo wakati wa mijadala wawasiliane na Katibu wa Baraza la Wawakilishi ili waweze kutoa huduma hiyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba serikali inawajibika kwa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Katiba. Ningeomba kujua kwa maagizo ya Kamati ya PAC ya mwaka jana ni maagizo mangapi serikali imewajibika kwa maagizo ya Kamati hiyo, kamati ambayo ni sehemu ya Baraza la Wawakilishi.

(b) Shughuli zetu hapa Barazani zinanoga sana kwa msaada wa waandishi wa habari hasa TVZ na STZ lakini waandishi wa habari hawa wanapata maposho madogo sana kupitia idara zao kwa maana ya Wizara ya Habari. Kwa nini serikali haiamui kwa makusudi kwamba waandishi wa habari wa TVZ na STZ ambao ndio wanaohuisha utendaji wa Baraza kupewa maposho na mafao ndani ya Baraza hili badala ya Wizara ya Habari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika,

(a) Kuhusu maagizo mangapi yaliyoagizwa na Kamati ya PAC kutekelezwa kwa wakati huu sina takwimu hizo na siwezi kuzitoa mbele ya Baraza lako hili tukufu. Ninachoamini maagizo mbali mbali yanayoagizwa na Kamati ima na Baraza hili serikali inayatekeleza vizuri. Inategemea sana uwezo wa serikali kwenye bajeti yake ili kutekeleza majukumu yale yote. Ni nia ya serikali hupenda watekeleze mambo yote lakini kutokana na hali yetu ya uchumi wakati mwengine huwa tunashindwa kufanya hivyo.

(b) Kuhusu upande wa waandishi wa habari. Mhe. Spika, serikali yetu ingependa sana kuona waandishi wetu wa habari na wafanyakazi wengine wanapata mishahara mizuri na maposho mazuri. Lakini kama nilivyosema awali kutokana na hali yetu ya kiuchumi haituruhusu kufanya hivyo. Hivi sasa kwa kuwa waandishi wa habari wanaajiriwa katika taasisi zao, kwa hiyo mwenye taasisi ndio mwenye haki ya kuwalipa waandishi hao. Ingakuwa serikali inao uwezo mkubwa tungetoa posho maalum kwao. Lakini kwa bahati mbaya kutokana na uwezo wetu mdogo wa kibajeti hatuwezi kufanya hivyo.

Ningependa kutoa wito kwa wananchi wote tuzidi kuzidisha juhudi za kuzalisha ili uchumi wetu ukue na tuwe na uwezo zaidi wa kuweza kuwashughulikia wananchi wote hasa wafanyakazi wetu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi kifungu (d) alitoa wito kwa vyombo vya habari kuja hapa Barazani kuonana na Katibu kwa ajili ya kupata nafasi ya kurusha vipindi moja kwa moja.

Mhe. Spika, tunavyoelewa kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari ina vyombo vyake inavyotumia yaani televishen na radio. Je, swali langu ni kwamba kwa nini Mhe. Waziri kwanza usivutumie vyombo vyako vya televishen na radio kwa ajili ya kurusha matangazo mbali mbali na badala yake ukatoa wito kwa vyombo vyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni furaha ya serikali kuvikaribisha vyombo vyake viweze kurusha matangazo moja kwa moja. Hii kama nilivyosema kutokana na ufinyu wa bajeti zetu ndio

tatizo la msingi linalofanya kushindwa kufanywa hivyo. Pale hali itakapokuwa nzuri tutaanza na vyombo vyetu na vyombo vyengine vyenye uwezo wa kufanya hivyo, tunavikaribisha kufanya hivyo ili kutoa taarifa vizuri zaidi kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba serikali inawajibika kwa Baraza la Wawakilishi katika mambo mengi. Baraza la Wawakilishi kupitia Kamati zake zinatumia fedha nyingi katika shughuli za Kamati. Lakini cha kushangaza ni kwamba watendaji wakuu wa serikali hawaonekani kuhudhuria wakati wa majumuisho ya Kamati yanapofanyika. Lakini tunawaona kwa wingi katika kupitisha bajeti.

Je, huu ndio uwajibikaji katika serikali wakati huo wa kupitisha maazimio ya Kamati ni wakati wa kuona kwamba serikali ina wajibika vipi kwa wananchi wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni wajibu wao watendaji wa serikali kushiriki kikamilifu katika Kamati hizi. Kama hawatekelezi wajibu huo tutaendelea kuwakumbusha ili watekeleze wajibu wao na washiriki kikamilifu. Naamini pale ambapo watendaji wakuu wakati mwengine wana shughuli nyengine lakini wapo wawakilishi wao wanafanya hivyo. Tutahakikisha kwamba mara zote watendaji wakuu waipe kipaumbele kushiriki katika Kamati hizi za Baraza kwa sababu ni jambo moja muhimu sana katika utekelezaji wa shughuli za serikali.

Nam. 147

Uchafuzi wa Maji ya Bahari Katika Fukwe

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa mfumo wa Maji taka katika Majengo, Viwanda na Mahospitali ya Unguja Mjini yanamalizia kwa kuwaga maji hayo yenye sumu na chemikali mbali mbali katika fukwe za bahari. Na kwa kuwa viumbe hai (BIOANWAI) vilivyomo baharini hutumia maji na takataka hizo kama chakula. Na kwa kuwa kuna mtegemeano wa chakula *(food chain)* baina ya viumbe vya bahari na hivi vya ardhini.

Je, serikali ina mpango gani wa kurekebisha mifumo hiyo ili kuwanusuru watu wasipate madhara kutokana na umwagaji huo wa maji machafu baharini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamo wa Kwanza wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 147 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mfumo wa ukusanyaji wa maji machafu *(sea rage system)* upo ndani ya Mji Mkongwe wa Zanzibar pekee katika eneo lote la Mji wa Zanzibar. Mfumo huu unakusanya maji machafu kutoka kwenye karo mbalimbali zilizopo kwenye maeneo ya mji huo. Ni kweli kuwa maji machafu yote yanayotoka eneo la Mji Mkongwe kutoka kwenye makaro hayo yanayomwaga baharini kupitia mitaro 27 inayoingia baharini yaani "*seaoutfalls*".

Mhe. Spika, mfumo huo wa kutumia mitaro ya maji machafu inayoingia baharini (*seaoutfalls*) ni mfumo ambao sio kamilifu kwa ajili ya kusafisha maji machafu kufikia viwango vya kimazingira vinavyohitajika. Hata hivyo ni mfumo unaosaidia kupunguza ukubwa wa athari za kiafya na kimazingira.

Mhe. Spika, kabla ya mwaka 1995, mitaro mingi ya maji machafu iliopo maeneo yote ya Mji Mkongwe ilikuwa inamwaga maji machafu kando kando mwa fukwe za maeneo mbali mbali za mji huo. Hali hiyo ilikuwa inasababisha kero kubwa kwa wananchi na inahatarisha afya ya jamii na mazingira kwa jumla.

Mwaka 1996, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza la Manispaa chini ya mradi uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) ilifanikiwa kuboresha hali hiyo kwa kuufanyia matengenezo makubwa mfumo wote wa mitaro ya maji machafu ndani ya Mji Mkongwe wa Zanzibar. Kufuatia matengenezo hayo mitaro inayoingia baharini ilipunguzwa kutoka mitaro 40 hadi 27 sambamba na kuongezwa urefu wa mitaro hiyo kuingia baharini. Hivi sasa urefu wa mitaro hiyo kuingia baharini ni kati ya mita 40 hadi 145 kutegemea na aina ya mtaro na sehemu uliopo mtaro huo. Hali hiyo imesaidia kupunguza makali ya uchafu huo na kuwa rahisi kutawanya kwa kutumia mawimbi na mwenendo wa maji ya baharini.

Mhe. Spika, mwaka 2010, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Baraza la Manispaa limefanya utafiti wa kujua namna gani bora ya kusafisha maji machafu yanayozalishwa ndani ya Mji wa Zanzibar. Utafiti huo umefanyika kwa msaada wa Benki ya Dunia ambao umetoa mapendekezo kadhaa ya mfumo unaofaa wa kusafisha maji machafu yanayozalishwa ndani ya Mji wa Zanzibar. Mapendekezo hayo yameshawasilishwa kwa Uongozi wa Baraza la Manispaa kwa hatua za kuhamasisha nyenzo za utekelezaji. Ni imani yangu kuwa mara nyenzo hizo zitakapopatikana basi tatizo hilo la kumwaga maji machafu yasiyofikia viwango vya kimazingira litaondoka.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika,

(a) Kwa kuwa Mji Mkongwe au mji wa Unguja Mjini ni miongoni mwa miji midogo sana katika miji ya nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Na kwa kuwa nchi nyingi tayari zimedhibiti maji taka yake ili kunusuru afya za wananchi wao. Je, kwa sababu Mhe. Waziri anasema kwamba utafiti umeshafanyika ni lini nchi yetu itaamua kuweka bwawa tu la kuyatibu maji (*treatment plans)* hatimaye kuyamwaga baharini yakiwa salama au kuyarudisha kwa wananchi kwa ajili ya matumizi mengine kama vile umwagiliaji maji na kuwapa mifugo.

(b) Je, kuendelea kufanya utafiti na kubaki tulivyo kama ilivyo sasa, yaani kuendelea kuyamwaga maji yenye taka na sumu baharini si kuzorotesha afya za wananchi wan chi hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika,

(a) Kama nilivyojibu katika jibu mama kwamba tayari tafiti zimefanyika. Na kuna mifumo mbali mbali ambayo tayari imetolewa kama ni *alternative* ya jinsi gani ya kuyashughulikia maji machafu ukiwemo huo ambao ameutaja yeye wa kujenga bwawa la ku- *treat* maji.

Lakini Mhe. Spika, naomba Mheshimiwa akubaliane na mimi kwamba uwezo wa kifedha ndani ya serikali yetu ni mdogo na miradi hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi. Ninachoweza kumuahidi ni kwamba serikali itafanya kila juhudi ya kutafuta wabia katika shughuli hii ili kuhakikisha kwamba maji hayo machafu yanashughulikiwa ipasavyo.

(b) Ni kweli kwamba serikali inajali sana afya ya wananchi wake na ingependa kwa kiasi kikubwa sana kuondosha athari hizo ndogo ndogo ambazo zinatokewa kwa kumwagwa maji machafu ndani ya bahari. Lakini bado Mhe. Spika, naomba Mheshimiwa avute subira, tatizo ni lile lile. Kujua sababu ni njia moja ya kuanza kuelekea jinsi ya kutafuta suluhisho. Naomba Mheshimiwa avute subira.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kama ilivyodhirika katika majibu kwamba eneo moja ambalo linaathirika sana na uchafuzi wa mazingira kupitia maji machafu ni eneo la Mji Mkongwe. Lakini mfumo huu wa kukusanya maji machafu na kuyapeleka baharini au katika maeneo mengine umekuwa

ukiathiriwa sana pia na kutokunzwa na mfumo wenyewe unapotokana na kuharibika kwa mifunuko ya maeneo haya au makaro.

Vile vile kutokana na kuharibika kwa sehemu hizi na kitendo cha kutokukusanywa taka kwa miezi kadhaa katika Manispaa ya Mji wa Zanzibar hasa katika Jimbo la Mji Mkongwe kunapelekea mataka haya kuingia katika makaro na kuathiri mfumo mzima wa kupeleka maji machafu kufika katika sehemu zilizokusudiwa.

Je, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imechukua hatua gani za kuwasiliana na Baraza la Manispaa kuona linatekeleza wajibu wake ili kuepuka uchafuzi huu mkubwa wa mazingira unaofanyika katika mji wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kwamba hutokea maharibifu ambayo baadhi yao husababishwa na wana jamii wenyewe kwa kutupa taka na kuzuia mifumo hiyo ambayo inapeleka maji taka baharini kwa ajili ya kuyashughulikia ipasavyo.

Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itashirikiana kikamilifu na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye ndiye anayehusika na Baraza la Mji, katika kuhakikisha kwamba mitaro hiyo inashughulikiwa katika matengenezo. Vile vile kuwahamasisha wananchi katika kutoa elimu kwamba ni muhimu kutunza mazingira yetu ili yasizidi kutuletea athari katika afya zetu.

Nam. 48

Madeni ya Serikali kwa Wahisani wa Maendeleo

Mhe. Omar Ali Shehe – Aliuliza**:-**

Katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo, na kutokana na umasikini unaoikabili nchi yetu, serikali yetu hulazimika kukopa fedha nyingi sana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, hali inayopelekea nchi yetu kulazimika kulipa madeni hayo makubwa kwa kila mwaka.

(a) Je, hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inadaiwa kiasi gani.

(b) Hali ya uwiyano wa ukopaji na ulipaji wa madeni hayo, ikoje kwa kila mwaka.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa heshima kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye sehemu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa mwakilishi kuwa katika kutekeleza mipango yetu ya maendeleo huwa tunahitaji misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo kupitia ruzuku na mikopo. Hali hii inatokana na kwamba kasi ya mahitaji ya maendeleo yetu haiendi sambasamba na mapato yetu ya ndani, hivyo kupelekea nchi yetu kulazimika kutafuta misaada ikiwa ni pamoja na mikopo nafuu ili kuweza kutekeleza mipango yetu ya maendeleo na hatimae kufikia malengo tuliyojipangia. Suala la kukopa sio kwa nchi zinazoendelea tu bali hata nchi zilizoendelea.

Mhe. Spika baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Februari mwaka 2011 Serikali ya Mapinduzi ya Zanizbar inadaiwa jumla ya Tsh. bilioni 152.1 Kati ya deni hilo la nje la ndani ni Tsh. bilioni 42.5 sawa na asilimia 27.9. Hata hivyo, ni asilimia 16.2 tu ya deni lote hilo linadhaminiwa na SMZ.

b) Mhe. Spika, kuhusu hali ya uwiano wa ukopaji na ulipaji wa deni la Taifa kwa kila mwaka, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa ni nzuri. Mikopo ya nje hulipwa kwa kipindi kirefu cha miaka 20 au zaidi. Kwa tafsiri zaidi mikopo hii hutoa nafasi kwa serikali kulipa kidogo kidogo.

Kwa upande wa deni la ndani, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huwa inalipa madeni hayo kila mwaka hutegemea Bajeti iliyopitishwa na Baraza lako tukufu. Hata hivyo baadhi ya deni la nje hudhaminiwa na hulipwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Deni la Taifa iwapo litagawanywa kwa Mzanzibari mmoja mmoja kila mzanzibari atakuwa anagaiwa kiasi gani?

Lakini kwa vile kunakuwa na ongezeko la makusanyo ya kodi kila mwaka katika nchi yetu. Ni kwa nini kasi ya utegemezi ya misaada ya mikopo haipungui. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, deni la taifa kama nilivyosema ni bilioni 152, idadi ya Wazanzibari ni milioni moja na laki tatu, ukitaka kuligawa kwa kila Mzanzibari ni bilioni 152 gawa kwa milioni moja na laki tatu, bahati mbaya sina *calculator*. Lakini namwambia Mheshimiwa akigawa hivyo atapata kila Mzanzibari deni lake ni kiasi gani. Kama ni suala la kupiga bakuli basi kila mzanzibari hapo utapata deni lake ni kiasi gani.

Suala la upungufu wa deni la Taifa. Nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi na Wazanzibari kwa ujumla deni kubwa ambalo tulokuwa nalo limetokana na mikopo ambayo tumeipeleka katika ujenzi wa miundombinu na hasa barabara, umeme, maji lakini sisi sote Wazanzibari ni mashahidi kwamba hali yetu ya barabara sasa hivi inaridhisha. Mikopo inayokwenda sasa hivi kwa miundombinu hasa ya barabara itapungua na kwa maana hiyo nataka nikuthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba kuanzia sasa mikopo yetu itaanza kupungua na hatimaye kila unapokuwa unaiva kwa sababu mkopo wa nje hulipi mpaka pale mkopo unapoiva, na mikopo yetu mingi sana *in a grass period* ya miaka mitatu mengine mpaka mitano inaanza kulipwa kidogo kidogo mpaka miaka ishirini tunamaliza. Nataka nikuhakikishie kwamba sasa mikopo yetu itaanza kupungua hasa kwa kutilia maanani kwamba Mhe. Rais Amani Abeid Karume alitilia mkazo sana ujenzi wa barabara na barabara nyingi zimeshajengwa sasa hivi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika miaka mwishoni ya 90 Tanzania ilinufaika kwa kuingiza katika mpango ule wa *Highly Injected Pure Countries* (*HIPC*) sasa kwa sababu Zanzibar ni moja ya nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na msamaha ule wa madeni ulipaswa pia kunufaisha. Je, kiasi gani Zanzibar imefaidika na msamaha ule ili kuweza kupunguza deni hili la Zanzibar ambalo linadaiwa hasa katika madeni ya nje.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana nae kwamba Tanzania ilifaidika katika *HIPC* na Zanzibar ni miongoni mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa upande wetu nataka nimthibitishie kwamba tulifaidika. Lakini kwa sababu alitaka takwimu sasa hivi sitakuwa nazo, lakini namuhakikishia nitampatia ili kuweza kufahamu ni kiasi gani na Zanzibar tulifaidika katika sehemu ile ya *HIPC*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri amekiri kwamba Zanzibar inadaiwa takribani bilioni mia na hamsini na mbili kama deni la ndani na nje ya nchi. Mimi naomba kujua deni hili ni pamoja na ule mchele ambao Zanzibar unadaiwa kutoka Thailand ambao limekuwa ni deni sugu na la aibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, labda ningelimuuliza Mhe. Mwakilishi ni mchele upi kwa sababu kuna michele mingi atoe ufafanuzi anotaka yeye kujibiwa ni mchele upi halafu ndio nimpe ufafanuzi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa kunisaidia kutoa ufafanuzi ni mchele ambao Zanzibar ulikopeshwa tangu mwaka 1988 ambao Balozi wa Tanzania nchini Malaysia wanaujua huu ndio ninaozungumzia mimi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nilimfahamu anataka mchele ule lakini kwa sababu nilitaka na wawakilishi wengine wajue ni mchele upi anao-*refer* yeye.

Mhe. Spika, nataka niseme tu ule mchele deni lile lina utata na sisi kama ni serikali tumechukua deni kwa maana ya *principle* tumeliweka kama ni deni tunalodaiwa, kile cha juu hatujakiweka kwa sababu kina utata.

Nam. 31

Kuthaminiwa kwa Wafanyakazi wa Masjala

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Aliuliza**:-**

Kama tunavyofahamu, Masjala ni sehemu muhimu kwa kila wizara na ina mchango mkubwa wa kuhifadhi kumbukumbu na kurahisisha mawasiliano ya ndani ya Wizara ama Taasisi husika. Hata hivyo, wafanyakazi wa sehemu hiyo hawathaminiwi na wanaonekana ni watu wa mwisho katika Wizara ama Idara za Serikali.

(a) Je, kuna sababu zipi zinazopeleka kuwepo kwa hali hiyo.

(b) Kwa nini wizara haiwapi fursa ya kubadilishana uzoefu baina ya wafanyakazi wa Masjala wa Pemba na Unguja.

(c) Kwa kuwa wafanyakazi hao wana umuhimu mkubwa. Je, Mhe. Waziri kwanini hawapewi kipaumbele kitengo hicho katika kuwapatia masomo ya muda mrefu na mfupi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba masjala ni sehemu muhimu kwa kila Wizara, Idara na Taasisi za Umma kutokana na mchango mkubwa ilionao wa kuhifadhi kumbukumbu na kurahisisha mawasiliano ya ndani na nje ya Wizara, Idara au Taasisi husika. Hata hivyo, naomba kidogo nitafautiane na mawazo ya Mhe. Mwakilishi kuhusu hadhi ya wafanyakazi wa sehemu hii. Katika kada ya Utumishi wa Umma wafanyakazi wote popote walipo wanatambuliwa na kuthaminiwa kwa mujibu wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hakuna kutothaminiwa kwa wafanyakazi wa masjala na kwa hivyo hakuna sababu za kuwaona wao ni watu wa mwisho katika Wizara ama Idara za Serikali. Kiutumishi, wafanyakazi wa masjala wana hadhi sawa kama wafanyakazi wengine wa Serikali.

(b) Mhe. Spika, nakubaliana na ushauri ulitolewa na Mhe. Mwakilishi wa kubadilishana uzoefu wa utekelezaji kazi wafanyakazi wa masjala kwa upande wa Unguja na Pemba. Hata hivyo, suala hili linahitaji maandalizi ya mipango na bajeti ili kukidhi gharama za maisha kwa watumishi watakaohusika na utekelezaji wa zoezi hilo kwa kipindi watachokuwemo kwenye shughuli hiyo. Wizara yangu inatoa wito kwa Wizara nyengine na taasisi mbali mbali za serikali kulizingatia wazo hili na kulifanyia kazi ipasavyo. Jambo la kuzingatia ni kwamba ziara hizo zilenge katika kubadilishana uzoefu na hatimaye kuleta tija kwa maslahi ya utumishi wa umma nchi kwa jumla.

(c) Mhe. Spika, kutokana na kuthamini mchango unaotolewa na watumishi wa masjala, Serikali kupitia Programu ya Marekebisho ya Utumishi wa Umma imeandaa mpango maalum wa kuwatambua watumishi hao kwa kuwawekea kada maalum ambayo itajali maendeleo yao tokea wanapoanza kuajiriwa kwa mara ya kwanza hadi watakapostaafu kazi.

Nam.134

Maandiko ya Kisheria Kuhusu Maridhiano

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Alijibu**:**

Kuna maridhinao yaliyofanywa na viongozi wetu wa Kitaifa ambayo yalipelekea
kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, ni jambo zuri sana linalostahili pongezi.

(a) Je, kuna maandiko yoyote ya Kisheria yanayoonyesha maridhiano hayo.

(b) Kama yapo je, tunaweza kupatiwa nakala ya maridhiano hayo ili kuweza kuwapatia wananchi waweze kujua.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 134 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba maridhiano yaliyofikiwa pale Ikulu baina ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk Amani A. Karume na Katibu Mkuu wa CUF Mhe.Maalim Seif Sharif Hamad, yalileta umoja nchini na kuweza kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hili ni jambo zuri.

Mhe. Spika, maridhiano ya viongozi hao wawili hayakuwa kwa maandishi. Maridhiano haya ni ya uungwana, ukweli, nia safi na uzalendo. Mbali na hayo ni kuwa mmoja wa waliofanya maridhiano hayo, kwa wakati huo alikuwa Rais wa Nchi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Yeye mwenyewe alitamka katika Mkutano wa Kibanda Maiti (Uwanja wa Demokrasia) kuwa wamekubaliana na Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif kuondoa tafauti zao na za vyama vyao na kuijenga Zanzibar yetu kwa pamoja katika misingi ya umoja, maelewano, udugu na usalama. Rais anaposema na kutamka jambo basi kauli hiyo huwa ni agizo kwa watendaji ili lifanyiwe kazi katika misingi ya agizo lenyewe. Na ndio maana Rais akisema jambo mara nyengine wananchi huandamana kwa kuunga mkono suala hilo na hata kuomba lifanyiwe sheria ili kulipa uzito zaidi.

Maridhiano haya ya Rais Amani na Maalim Seif, yaliungwa mkono vile vile. Hata Baraza lako tukufu Mhe. Spika, liliunga mkono kwa kupitisha Azimio Barazani ambalo liliagiza mambo kadha, ikiwemo kufanyika kura ya maoni na kuundwa kwa serikali ya Umoja wa Kitaifa pamoja na kurekebishwa kwa Katiba ya Zanzibar ili maridhiano hayo sasa yatekelezwe kisheria (Kikatiba) kwa sabau ya uzuri wa jambo lenyewe na kuweza kuwa na usalama, umoja na uzalendo wa kujenga Zanziabar yetu.

Mhe. Spika, kwa sababu hizo basi, maridhiano hayo sasa yamewekwa kwa kimaandishi ndani ya Katiba yetu ambayo sasa yamekuwa ni Sheria Kuu.

b) Mhe. Spika, kutokana na maelekezo ya hapo juu kila Mzanzibari ni wajibu wake kuisoma Katiba ya Zanzibar ili ajue kwa undani maridhiano hayo na faida yake, kama yakivyoelezwa ndani ya Katiba yenyewe. Vile vile ni jukumu letu sisi viongozi, na hususan Waheshimiwa Wawakilishi kutoa elimu hiyo ndani ya majimbo yetu ili wananchi wetu waelewe kwa undani maridhiano hayo na faida iliopatikana kutokana na maridhiano yenyewe.

Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Mtando ni Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni na kwa sababu suala hili analielewa vyema basi natoa wito kwake awaelimishe wananchi wa jimbo lake kwa maslahi yao na taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza kabla ya kuuliza nitoe pongezi kwa Mhe. Waziri kwa namna alivyolijibu hili swali vizuri sana.

Mhe. Spika, palipigwa kura ya maoni na wananchi wakaamua kuwa na muundo mwengine wa serikali na baada ya kubadilisha Katiba ndio ikapatikana Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa ambayo Mawaziri wake wanatokana na uwiano wa kura zilivyopatikana katika majimbo kupitia Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, maridhiano haya yalikuwa kwa kuunda hii ngazi ya juu tu ya Baraza la Mawaziri pamoja na Urais lakini hakukuwa na mpango wowote madhubuti uliowekwa kwa hizi ngazi za chini kama Wakurugenzi, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na kadhalika. Kama upo unapita kwa maridhiano au vipi mimi nataka kujua hilo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, Katiba ni sheria mama na haiwezekani si hapa Zanzibar tu lakini nchi yoyote haiwezekani kuwa kila makubaliano mkayaweka katika Katiba, lakini Katiba unaweka msingi mkuu

wa zile shughuli ambazo mnataka kuzifanya. Kwa maana hiyo Katiba yetu imeweka msingi mkuu na msingi mkuu ni kuonesha kwamba ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa na huo ndio msingi mkuu ambao unatakiwa utekelezwe kwa utaratibu ambao viongozi wanaohusika wataona inafaa. Hata katika hayo waliyoyasema Wakurugenzi na wengine naamini kwamba serikali imetilia maanani sana na imechukua hatua hizo na wametekeleza kwa mujibu wa utaratibu ambao umekubaliwa.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri. Je, haoni kwamba maridhiano kutokuwa na maandiko hilo hawaoni kwamba huko mbele linaweza kuleta utata na kero kama zile za muungano.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nilisema kwamba maridhiano hayo hapo mwanzo hayakuwa kwa maandishi yalikuwa ni makubaliano ya kiungwana, ya ubinadamu na kuridhiana. Lakini baadae yakawekwa kimaandishi katika Katiba, sasa Katiba ndio sheria kuu na ndio maandiko makuu ya nchi. Kwa hivyo, maridhiano yote hayo yaliyokubaliwa sasa hivi yamo katika Katiba na Katiba hii tuliipitisha hapa hapa mbele ya Baraza lako hili tukufu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, maridhiano hayo sasa yapo kimaandishi na naamini kwamba haitakuwa matatizo kwa sababu tutafuata matakwa ya Katiba yanavyosema.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa katika hayo marekebisha yetu sasa hivi tunaita Serikali ya Mapinduzi lakini vile vile kwenye Katiba yetu tuna marekebisho yanaitwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Je, utakubaliana na mimi kuwa tuondowe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tuweke Serikali ya Kitaifa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, Katiba yetu imetambua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hili ndilo jina la Serikali na imetambulika Kikatiba, lakini katika makubaliano tulisema kwamba Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa na Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo, usahihi hasa tunaweza tukasema kwamba ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa.

Nam. 29

Serikali Kuanzisha Maghala ya Karafuu Nje ya Nchi

Mhe. Abdalla Moh'd Ali - Aliuliza**:**

Kwa kuwa zao la karafuu hivi sasa lina soko kubwa sana ulimwenguni, na kwa kuwa Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) tayari limeshaanzisha ghala la Karafuu katika nchi ya Dubai.

(a) Je, Kuna faida na hasara zipi zinazopatikana kwa Shirika hilo kuendeleza uhifadhi na uuzwaji wa Karafuu kupitia ghala hilo la Dubai.

(b) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuanzisha ghala kama hizo katika nchi nyengine, ili kukuza faida na kutanua soko zaidi.

(c) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuiga utaratibu huu kwa bidhaa nyengine zinazozalishwa hapa Zanzibar, ikiwa ni pamoja na mwani na viungo (*spice*) mbali mbali.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 kwa kuanza na utangulizi ufuatao:-

Mhe. Spika, ni kweli zao la karafuu hivi sasa lina soko kubwa sana ulimwenguni, hata hivyo soko hili kwa kiasi kikubwa limekuwa likihodhiwa na wafanyabiashara wa kati (*middle businessman*) badala ya watumiaji (*consumers*). Vile vile athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi ambazo zimeanza kujitokeza katika nchi zetu zimesababisha kuwa na hali ya mavuno yasiyoweza kutabirika na kufanya kuwepo kwa uhaba wa zao lenyewe la karafuu miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa zao hilo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kuwepo ghala la karafuu katika nchi ya Dubai kuna faida kubwa itokanayo na karafuu hizo kuwafikia watumiaji wa mwisho na hivyo kupata bei kubwa, lakini pia kuweza kuuza hata kwa viwango vidogo vidogo kwa kadiri ya mnunuzi atakavyo.

Kwa upande wa hasara ni pale *ZSTC* inaposhindwa kupeleka karafuu katika ghala hilo kutoka Zanzibar kutokana na uhaba wa karafuu zenyewe, suala ambalo kwa sasa Serikali imo katika mikakati ya kulifanyia marekebisho Shirika lenyewe pamoja na uendelezaji wa zao la karafuu.

(b) Mhe. Spika, kuanzishwa kwa maghala au afisi kama hizi katika nchi nyengine kutategemea zaidi kuwepo bidhaa hiyo ya kutosha na vile vile gharama za uendeshaji katika nchi husika yakiwemo pia masharti nafuu ya uhaulishaji wa fedha kutoka nchi hiyo kuja Zanzibar bila ya usumbufu, sharti ambalo ndio msingi mkuu wa kuanzisha afisi ya biashara nje ya nchi, ukiwacha lile la kuzitangaza na kuzisogeza zaidi bidhaa zetu karibu na masoko.

(c) Mhe. Spika, kuiga utaratibu huu kwa bidhaa nyengine kama mwani na viungo (*spices*) mbali mbali si tatizo, ila tu suala la msingi ni kuwepo kwa bidhaa hizo kwa mujibu wa soko linavyohitaji.

Mhe. Spika, tofauti na zao la karafuu ambalo huuzwa nje ya nchi kama bidhaa kamili (*finished product*), zao la mwani huuzwa viwandani likiwa ni mali ghafi (*raw material*) hivyo si rahisi hata kidogo kuuzwa katika masoko kama karafuu.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kuna mipango ambayo imeandaliwa ya kuzifanyia marekebisho Shirika la Biashara ili kuyafunga masoko hayo na kwa hivi sasa zao la karafuu kama ulivyosema limekuwa ni la msimu. Sasa sijui ni lini hili Shirika litalifunga soko hili ili kupunguza mzigo kwa Shirika hili la *ZSTC*.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa sasa linafanya mapitio makubwa ya Shirika la *ZSTC*, mapitio ambayo kwamba yataliweka Shirika hilo liwe imara na linaweza kufanya biashara zake bila ya matatizo yoyote. Kwa hivyo, suala la kwamba kuna kufunga soko na kufungua soko hilo bado mpaka tumalize kazi ya mapitio ya Shirika zima kuanzia sheria yake, muundo wake mpaka masuala ya masoko kwa dunia nzima. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi awe mvumilivu kidogo katika kipindi kifupi tu basi ripoti hiyo itafika mpaka hapa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mlinde Mbarouk Juma: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa ghala la karafuu liko nchini Dubai ni wafanyakazi wangapi wa Zanzibar wanaofanya kazi katika ghala hilo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, Dubai tuna Afisi ndogo na ghala ndogo inaweza kuhifadhi tani kama mia saba za karafuu na kuna wafanyakazi wanne.

Nam. 75

Wizara Kuimarisha Maslahi ya Walimu

Mhe. Rufai Said Rufai - Aliuliza**:**

Mnamo mwezi wa April, 2010 Serikali kupitia mabadiliko ya Mpango wa Ajira za Watumishi wa Serikali (*Scheme of Service*) iliamua kuongeza maslahi ya walimu. Hata hivyo, jambo la kusikitisha, sasa ni miezi kumi imepita kuna baadhi ya walimu bado hawajafanyiwa marekebisho hayo.

(a) Je, ni lini walimu hao waterekebishiwa mishahara yao.

(b) Ni nini kilichosababisha kutofanywa kwa marekebisho hayo.

(c) Kwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara aliahidi kulipwa malimbikizo ya mishahara ya walimu hao; Ni lini italipa mishahara ya walimu hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 lenye vifungu (a), (b) na (c) kabla ya hapo Mhe. Spika, ningependa kutoa maelezo ya ufafanuzi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika mwezi April, 2010, Serikali iliamua kuwarejesha walimu asilimia 25 ya posho la kufundishia na kuwaingiziwa katika mishahara yao. Kutokana na kuingizwa kwa asilimia 25 ya posho la kufundishia katika mishahara ilisababisha mishahara ya walimu wote ifanyiwe marekebisho. Marekebisho hayo yalifanywa kwa walimu wote na wala sio sahihi kwamba baadhi ya walimu hawakufanyiwa.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa walimu wanafahamu namna mabadilko hayo yalivyofanywa, wizara ilionana na walimu wote katika Wilaya zao na kuwapa maelezo na kuwataka waipitie mishahara yao na wale walio na malalamiko ya kuongezewa au kupunguziwa waiarifu wizara mara moja. Wizara iliyafanyia kazi malalamiko yaliyowasilishwa kwa kuhakiki taarifa zote zilizowasilishwa na kugundua kuwa jumla ya walimu 100 walipewa mishahara mikubwa kuliko walivyostahiki na walimu 311 walilipwa mishahara ya chini kuliko walivyostahiki. Baada ya kukamilika kwa zoezi hilo wizara iliarifu rasmi Idara Kuu ya Utumishi Serikalini ambayo nayo iliarifu Wizara ya Fedha na Uchumi kuchukua hatua ya kufanya marekebisho yote kwa barua yao ya tarehe 5 Novemba, 2010.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutoa majibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, marekebisho ya mishahara ya baadhi ya walimu waliopewa mishahara midogo kuliko walivyostahiki yamefanyiwa marekebisho katika mishahara yao ya mwezi Februari, 2011. Kwa baadhi ya walimu ambao marekebisho hayo hayakufanyika yatafanyika katika mishahara yao ya mwezi Machi 2011.

(b) Mhe. Spika, marekebisho ya mishahara ya walimu waliolipwa kasoro yalichelewa kutokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na walimu wenyewe kuchelewa kutoa taarifa sahihi. Kutokamilika kwa taarifa za baadhi ya walimu na utaratibu mzima wa uhakiki kufanyika kwa hatua ukihusisha Wizara na baadaye Idara Kuu ya Utumishi Serikalini na hatimaye Utumishi kuiarifu Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuchukua hatua. Uhakiki huo unafanyika kwa tahadhari kubwa ili kuepuka kulipwa mshahara asiostahiki kwa baadhi ya wafanyakazi.

© Walimu wote watalipwa malimbikizo ya marekebisho ya mishahara baada ya kukamilika kwa marekebisho ya mishahara ya walimu wote 311. Ahadi ya kuwalipa malimbikizo mishahara kama ilivyoahidiwa na Naibu Katibu Mkuu kwa niaba ya wizara, itatekelezwa mara tu zoezi hili litakapokamilika. Ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kupata majibu hayo kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri. Lakini kwa kuwa haki ikichelewa kutolewa ni sawa na kuwa haikutolewa kabisa. Je, serikali ina mpango gani endelevu wa kuondosha kasoro hizi pale zinapotokea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kuchelewa kutoa haki ni sawa sawa na kumnyima mhusika haki. Lakini Mhe. Spika, kama tulivyoahidi, tunajua idadi kubwa ya walimu ambao tunao na uwezo wetu wa kifedha serikalini. Kwa hivyo, kama nilivyojibu katika swali mama napenda kusisitiza kama malimbikizo yote yale yaliyobakia ambayo tumeanza kuyalipa mwezi huu wa Febuari, 2011 tutahakikisha itakapofika mwezi wa Aprili tayari walimu wote watakuwa wamelipwa malimbikizo yao.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri hivi sasa kuna malalamiko makubwa ya walimu kuhusiana na huduma ya likizo. Kuna walimu wengi wanalalamika kwamba inatimia miaka 10 mpaka 15 hawapati huduma ya likizo, lakini kuna baadhi ya walimu kila mwaka takriban wanapata huduma

hii ya likizo. Je, kuna utaratibu gani unaotumiwa na wizara yako kuwakidhia walimu hawa huduma hii ya likizo katika usawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kuhusu suala la likizo kwa walimu ni kweli malalamiko hayo yapo kwa walimu wetu, lakini pia ifahamike hatuwezi kutoa likizo kwa walimu wote kwa mara moja, tunatoa likizo kwa utaratibu na walimu ambao tunawapa likizo pia tunawapa pesa za kwendea likizo kwa utaratibu vile vile.

Nam. 59

Kisima cha Maji katika Jimbo la Matemwe

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:

Kwa kuwa kisima cha maji kilichopo eneo la Kiashange huko Matemwe, Zanzibar kwa sasa kimeharibika na hivyo kuwafanya wananchi wa baadhi ya vijiji viliopo Matemwe kama vile Mikuuni, Mlilile, Kigomani, Kilima Juu na Kachongwe kukosa maji safi na salama.

Je, ni lini kisima hicho kitafanyiwa matengenezo ili kuwaondoshea wananchi wa maeneo haya usumbufu mkubwa wanaoupata kwa kukosa huduma hiyo katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, matengenezo katika kituo hicho yanaendelea na mafundi wamefika na kutoa pampu kwa matengenezo, baada ya pampu kutolewa kisimani imefanyiwa matengenezo ya awali. Hata hivyo, katika majaribio haikuweza kufanya kazi kama inavyotakiwa. Kwa hivyo, hadi sasa mafundi wamo katika matengenezo ya hitilafu iliyojitokeza na hatimaye kuirejesha kisimani kwa kupatiwa wananchi wa maeneo hayo huduma ya maji safi na salama.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa Kisima cha Kiashange ni tegemeo kubwa la maji katika Wilaya yetu ya Kaskazini ‘A’ na kinaonekana hivi sasa kimeshakuwa kinazidiwa na watu. Je, serikali ina mpango gani wa kuchimba visima vingine kwa ajili ya kukidhi haja hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, tatizo la maji kwanza haliko Matemwe tu, au katika visima vya Kiashange isipokuwa ni tatizo sugu kwa sasa hivi. Serikali kupitia wizara yangu baada ya kuliona tatizo hilo tayari tumeshafunga mikataba na mradi wa *ADB* ambao utashughulikia kujenga laini mpya za maji pamoja na kuchimba visima vipya katika maeneo ya Kiashange na Tunguu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini Mhe. Spika, kwa muda mrefu serikali yetu imekuwa ikifanya jitihada kubwa za kutoa fedha nyingi kuchimba visima pamoja na wahisani. Hivi karibuni tulipata msaada wa ndugu zetu wa Japani kuchimba visima vingi tu, lakini kinachoonekana visima vingi vinavyochimbwa vinakuwa havidumu kwa kuharibika au kukauka maji na imekuwa taifa letu linapoteza gharama kubwa bila ya mafanikio.

Ni nini hasa sababu za msingi zinazopelekea kutokuwa na utaalamu wa kuchimba visima vilivyokuwa endelevu na vilivyokuwa bora kuweza kutatua kero za wananchi wetu katika suala la maji hapa Zanzibar. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati niruhusu nimjibu Mhe. Ali Salum swali lake kwa swali mama nambari 59.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji wana vifaa, utaalamu wa kutosha wa kujua mali yalipo na maji kiasi gani. Kwa hivyo, mwahali wanamochimba huwa hawabahatishi na mara nyingi utakuwa kwamba kuna visima vya namna mbili, kuna visima vinaitwa *test bow holes*, ambavyo hivi huwa ni vingi tu. Lakini kimoja katika hivyo huwa ni *production bow hole* (ni kisima kitakachotumika kwa kutoa maji kwa ajili ya watu). Kwa hivyo, wanapoamua kutumia kisima hicho ni kwamba wameshafanya utafiti wa kutosha kutokana na visima mbali mbali, maeneo mbali mbali lakini ya karibu ya kisima hicho.

Kwa hivyo, kisima kukauka inategemea hali ya hewa, kukauka kwa kisima kuna sababu nyingi, moja ni kupatikana kwa mvua. Kwa sababu maji yaliyoko ardhini ndio maji pekee tunayotumia Zanzibar kwa ajili ya shughuli zetu zote. Kwa hivyo, inapotokea kuna ukame wa muda mrefu ni kweli visima hivyo hukauka na utaalamu wetu hautuoneshi kwamba mvua italetwa lini, ni kiasi gani cha maji kitaingia ardhini? Kwa hivyo, suala la kuharibika kwa kisima ni mazingira ya kawaida ya kimaumbile.

Jengine vile vile unaposema kuharibika au kukauka ni vitu tofauti, kuharibia Mhe. Spika, inategemea ardhi ilivyo. Katika visima vya *bow hole* huwa tunatumia vitu vinaitwa chungio, hivi mara nyengine huwa ni vya plastiki na mara nyengine huwa ni vya chuma. Vile vya chuma vinaota kutu, kutu ni maji na hewa, sasa vitu hivi viwili kama pana maji halafu maji yale yakaondoka ikiingia hewa kunatokea *oxidation*, hivyo vichungio vilivyofanywa kwa chuma vinamung'unyuka na hatimaye vinakuwa ni vibovu. Kwa hivyo, ardhi kwa sababu ya *pressure* inaisukuma na vinaharibika inakuwa kisima kinajifukia. Sasa nasema huu ni utaalamu mkubwa, lakini suala la *ZAWA* kuwa na uwezo na vifaa vya kujua kuna maji kiasi gani huo upo na wala hawabahatishi. Nakushukuru Mhe. Spika.

Nam. 64

Udhibiti wa Maadili katika Uendeshaji wa Sekta ya Utalii

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad - Aliuliza:

Kwa kuwa Utalii ambao ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya uchumi wa Zanzibar umekuwa ukisababisha mmong'onyoko wa maadili mazuri ya Zanzibar kutokana na watalii wengi wanaoingia nchini kinyume na maadili hayo na silka za Zanzibar.

Je, serikali ina mpango gani wa kuchukua hatua madhubuti na zinazotekelezeka, kuhakikisha hali hiyo ya mmong'onyoko wa maadili inadhibitiwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, nashukuru kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 64 lenye vifungu a, b, na c kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, mpango tulionao wa kudhibiti mmong'onyoko wa maadili unaosababishwa na ukuaji wa utalii Zanzibar ni kama huu ufuatao:

Kwa kuwa utalii umeingia kwa kasi kubwa imekuwa sio kazi rahisi kudhibiti maadili na silka za Mzanzibari kwa haraka. Hata hivyo, hatua mbali mbali zinachukuliwa na Kamisheni ya Utalii ili kutatua tatizo hili kutokana na kwamba sekta hiyo imemilikiwa na watu binafsi ambao wanazingatia zaidi maslahi yao ya kibiashara kuliko maadili na silka za nchi. Pamoja na hali hiyo, serikali imekuwa ikijitahidi kudhibiti mmong'onyoko wa maadili na silka katika namna zifuatazo:-

a) Kuzidisha ushirikiano uliokuwepo kati ya Kamisheni ya Utalii na Kamisheni ya Utamaduni katika kuhakikisha kuwa hatua madhubuti zinachukuliwa ili kurudisha hadhi ya maadili ya Mzanzibari.

b) Kupitia mpango wa utekelezaji wa kazi wa Kamisheni ya Utamaduni, serikali inaendeleza Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari kila mwaka kwa makusudi ya kuelimisha jamii juu ya maadili na silka njema za Kizanzibari kwa wenyeji na wageni kutoka nje ya nchi.

c) Katika kudhibiti maadili na silka za Mzanzibari, Kamisheni ya Utamaduni inaendelea kutumia vyombo vyake vya kiutendaji ambavyo ni Baraza la Utamaduni na Sanaa, Baraza la Kiswahili na Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonyesho kwa ajili ya kuulinda, kuelimisha, kuuenzi na kuendeleza utamaduni wetu ambao ni rasilimali kubwa ya nchi yetu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. pamoja na majibu yake mazuri ni vijiji vingapi hivi sasa vimeanza kuathirika na huo mmong'onyoko wa maadili ya Kizanzibari. Halafu je, wizara yake ina msaada gani katika vijiji hivyo ambavyo vimeathirika na huo mmong'onyoko wa maadili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Waheshimiwa wajumbe ni lazima tukubali kwamba utalii ni tatizo na wataalamu wanasema utalii ni *double edge sword* maana yake ni upanga wenye makali sehemu zote. Kwa maana hiyo ni kwamba, kwa vyovyote lazima tutaathirika tu hatuna jinsi, kubwa ni kuangalia kiasi gani kuasirika huko. Dhana nzima ya awali juu ya utalii ilikuwa ni kuyaweka mahoteli yote mbali na miji, ile ilikuwa ni *concept* ya kuepusha wana jamii maana yake wasiingiliane na mahoteli. Kwa sababu tunajua kwamba utalii ni *double edge sword*. Kwa hivyo, kwa vyovyote suala la kuathirika ni lazima.

Lakini pamoja na hivyo, sisi kama wizara tunajaribu kukaa na Kamisheni ya Utalii pamoja na Kamisheni ya Utamaduni kama nilivyoeleza awali ili kuweka *code of conduct* kwa watalii wote wanaoingia nchini, Bandarini na *Air port* ili kuwapa zile waelewe kwamba wanaingia nchini hapa lakini masharti yetu ni haya. Hilo si suala zito kwa kweli, kwa sababu ni suala ambalo lilikuwepo toka mwanzo wakati wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, mtalii alikuwa akifika tu pale anapewa ile *code of conduct* kwamba bwana unaingia hapa lakini sisi masharti yetu ni moja, mbili, tatu, nne na wawalikuwa wanafuata

kwa sababu mtalii anapofika yeye si mtu mkaidi, yeye akifika anakuuliza vipi nivae hivi inaruhusika? Sasa inategema na sisi wenyewe.

Kwa hivyo, hilo suala kwa kweli tuko na Kamisheni ya Utalii kuliwekea mikakati, naamini kwamba baadae hilo suala mtaliona. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spaika, kwa sababu serikali ya awamu ya kwanza iliyokuwa inaongozwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume iliweza kuhifadhi mila na silka za Wazanzibari kwa kuweza kudhibiti haya mambo ya kuingia wageni humu hususan katika mavazi kwa kuwapatia Wazungu…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kikao nakiahirisha kwa muda mpaka umeme utaporudi.

(Saa 4:10 Baraza liliahirishwa kwa muda kutokana na kuzimika kwa umeme)

(Saa 4:32 Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wote ambao baada ya umeme kukatika tulikuwa tunafanya mawasiliano na Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme. Ametueleza kwamba, kumetokea dharura kubwa na wamelazimika kuzima umeme. Hivyo, umeme tulionao sasa hivi ni wa jenereta yetu ya *standby* ambayo haikidhi kuendesha mfumo wa hewa humu ndani, unaweza kuwasiliana pamoja na taa. Sasa kuendesha shughuli zetu bila ya mfumo wa hewa itatuletea tatizo. Shugnuli hiyo itachukua kiasi ya saa moja na zaidi kurekebisha hilo tatizo, kwa maana hiyo tukubaliane kwamba shughuli zetu tusitishe kutoka hapa ili twende kwenye shughuli za sala ya Ijumaa na baadae turudi jioni. Hivyo, naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 4:35 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula (MTAKULA) Nam. 3 ya mwaka 1988

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia sisi Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar kufika hapa tukiwa wazima wa afya na siha na *inshaallah* kwa uwezo wake ataendelea kutujaalia mafanikio katika shughuli zetu.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba niwasilishe mbele ya Baraza hili tukufu Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula (MTAKULA) Nam. 3 ya mwaka 1988 na Kutunga Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, mapendekezo haya ya kuanzishwa kwa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe ni katika hatua za kutekeleza sera ya uhakika wa chakula na lishe ya mwaka 2008 ambayo imeelekeza kuwapo kwa sheria itakayosimamia utaratibu wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe Zanzibar.

Mhe. Spika, madhumuni ya waraka huu ni kutoa ufafanuzi wa vipengele mbali mbali vya sheria hiyo ikiwemo mapendekezo ya muundo wa taasisi ambazo zimependekezwa kuanzishwa kisheria kwa lengo la kusimamia na kutoa muongozo juu ya utekelezaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe. Lengo ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inajihakikishia usalama wa chakula na lishe bora na ina uwezo wa kukabiliana na hali tete ya upungufu wa chakula na janga la njaa kwa kuweka mikakati na mipango thabiti ya kisera na kisheria.

Aidha, waraka huu unafafanua majukumu ya taasisi mbali mbali juu ya utekelezaji sambamba na kutoa mapendekezo ya kufutwa kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 1988 ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula.

Mhe. Spika, sababu zilizopelekea kwa kufutwa kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 1988 ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula ni kama hivi ifuatavyo:

Upeo wa Sheria ya MTAKULA ulielekeza katika kuongeza uzalishaji wa ndani na serikali ndio ikawa mshiriki mkuu katika uzalishaji. Hali hii ni kinyume na sera ya sasa ya kiuchumi huria ambapo sekta binafsi na wananchi ndio wazalishaji na serikali ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kisera na kisheria.

Sheria ya MTAKULA ilizingatia suala la uzalishaji pekee. Hata hivyo, dhana ya uhakika wa chakula na lishe inajumuisha kuongeza uzalishaji sambamba na kujenga uwezo wa wananchi hasa wa kipato cha chini kujinunulia chakula na kushajihisha matumizi sahihi ya chakula kwa afya bora ya mlaji.

Sheria ya MTAKULA ilielekeza mfumo wa upangaji wa malengo na utekelezaji ulioihusisha serikali kuu pekee hali ambayo ni kinyume na mtazamo wa sasa wa maendeleo unaoshajihisha ushiriki wa jamii katika mipango na utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Utekelezaji wa Sheria ya MTAKULA ulifuata mfumo wa chama kimoja hali ambayo inahitaji kubadilishwa kulingana na mabadiliko ya kisiasa ya hivi sasa.

Pamoja na sababu hizi, zipo pia sababu za msingi zilizopelekea kuanzishwa kwa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Kama nilivyokwisha tangulia kutaja hapo awali Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe imetayarishwa ili kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya mwaka 2008 ambayo inalenga kwenye mambo yafuatayo:

Kuongeza uwezo wa kuwepo kwa chakula kwa kuongeza uzalishaji kwa chakula cha ndani ya nchi na kufanikisha masuala ya biashara na masoko.

Kuongeza uwezo wa wananchi hasa wa kipato cha chini wa kupata chakula cha kutosha.

Kupunguza hali tete ya kutokuwa na uhakika wa chakula kwa jamii maskini na kuweka mikakati thabiti kwa ajili ya kutoa hifadhi kwa jamii na kulifanya taifa kuweza kujiweka tayari na majanga ya upungufu wa chakula na njaa.

Kufanikisha matumizi endelevu ya rasilimali za ardhini na baharini kwa ajili ya kutunza na kufanya mazingira yetu kuwa endelevu.

Mhe. Spika, rasimu ya Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe inapendekeza kwa kuanzishwa taasisi zifuatazo:

1. Baraza la Taifa la Kusimamia Uhakika wa Chakula na Lishe *(National Food Security and Nutrition Council).*
2. Baraza la Taifa la Kusimamia Uhakika wa Chakula na Lishe limependekezwa kuanzishwa kama ilivyotajwa kwenye kifungu namba 5 (1) cha rasimu ya mswada nilioulete mbele ya Wajumbe wa Baraza hili.
3. Baraza hilo ndio litakuwa chombo kikuu kitakachokuwa na jukumu la kusimamia kwa karibu utekelezaji wa kisera na programu kwa uhakika wa chakula na lishe kwa lengo la kuhakikisha kuwa Zanzibar kwa wakati wote ina uhakika wa chakula na kila Mzanzibari ana haki ya kupata chakula na lishe

bora ikiwa ni haki ya msingi ya kuishi maisha salama na yenye afya.

4. Baraza litakuwa na jukumu la kutoa miongozo na ushauri kwa taasisi zenye dhamana ya kusimamia masuala ya uhakika wa chakula na lishe.
5. Baraza hili pia litakuwa ndio chombo kikuu chenye kutoa maamuzi juu ya ugawaji wa chakula cha dharura kwa wananchi kutoka katika Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(Zanzibar Food Reserve)* pale inapotokea jamii imekabiliwa na njaa kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao.

Mhe. Spika, muundo wa Baraza ni kama hivi ifuatavyo:

Baraza hili litakuwa chini ya Makamo wa Pili wa Rais akiwa ni Mwenyekiti na Wajumbe watakuwa Mawaziri kutoka Wizara ambazo zinahusika na utekelezaji wa Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe kama ilivyo kwenye kiambatisho namba 1. Wakuu wa Wilaya, Wawakilishi wawili kutoka Kamati Tendaji ya Kusimamia Masuala ya Uhakika wa Chakula na Lishe na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili akiwa Katibu wa Baraza.

Sekretarieti ya Baraza la Taifa la Kusimamia Uhakika wa Chakula na Lishe. Sekretarieti ya Baraza la Taifa la Kusimamia Uhakika wa Chakula na Lishe imependekezwa kuanzishwa kama ilivyotajwa katika kifungu namba 8 cha Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe, ikiwa na majukumu makuu ya kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Taifa na kufanya tathmini ya hali ya chakula nchini na kutoa ushauri kwa Baraza kuhusiana na hali hiyo. Sekretarieti itakuwa chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili ambaye atakuwa ni Mwenyekiti na Wajumbe wake watakuwa ni watendaji kutoka Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

Mhe. Spika, chombo chengine ambacho kimependekezwa kuanzishwa na Mswada wa Sheria hii ni Kamati Tendaji. Mhe. Spika, Kamati Tendaji itakuwa ni chombo cha ushauri kwa Baraza na Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe kama ilivyopendekezwa kuanzishwa katika kifungu namba 9 cha Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

Majukumu makuu ya Kamati Tendaji ni kuongoza, kuelekeza na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa kazi, miradi na programu mbali mbali zilizotayarishwa kwa lengo na kutekeleza Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya mwaka 2008.

Kamati hii itakuwa na muundo utakaowajumuisha washiriki mbali mbali ambao taasisi zao kwa njia moja au nyengine zinahusika katika utekelezaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe.

Wajumbe wa Kamati ni kama hawa ifuatavyo:

1. Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili atakuwa Mwenyekiti.
2. Mkurugenzi Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe atakuwa Katibu.
3. Makatibu Wakuu kutoka Wizara mbali mbali kama zilivyoainishwa kwenye kiambatisho namba 1 ambacho wajumbe nyote mnacho wakiwa ni wajumbe wa kamati hii.
4. Afisa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya inayohusika na Kilimo na Biashara atakuwa mjumbe.
5. Afisa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya zisizo za Kiserikali nae atakuwa mjumbe.

Mhe. Spika, chombo chengine ambacho kimependekezwa kuanzishwa na mswada huu wa sheria ni Idara ya Uhakika wa Chakula lakini idara hii kwa mujibu wa mamlaka aliyonayo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameshaianzisha alipounda serikali yake.

Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe imependekezwa kuanzishwa katika kifungu namba 13 (1) cha mswada huu na itakuwa na majukumu ya kuratibu utekelezaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe katika ngazi ya taifa na wilaya. Idara hii pia itakuwa inafanya kazi kama Sekretarieti ya Baraza la Taifa la Uhakika wa Chakula na Lishe kama ilivyoelezwa katika kifungu nilichokwisha kukitolea ufafanuzi hapo awali.

Kimuundo idara itaendeshwa na Mkurugenzi na itakuwa na idadi ya wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji ya idara hiyo. Aidha, idara hii pia itakuwa na majukumu ya kuratibu mahusiano na taasisi nyenginezo ambazo zinahusika na utekelezaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe. Katika kuhakikisha hili kutakuwa na *focal person* katika kila wizara kama ilivyoelezewa katika kiambatisho namba 1 ambao watakuwa na jukumu la kuunganisha taasisi zao na idara hii.

Kamati za Uongozi za Wilaya zimependekezwa kuanzishwa katika kifungu namba 17 (1) cha mswada huu wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe na zitakuwa na majukumu ya kusimamia utekelezaji wa kazi mbali mbali zinazohusiana na uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za wilaya na shehia.

Muundo wa kamati utajumuisha Mkuu wa Wilaya ambaye ndio atakuwa Mwenyekiti na Afisa Tawala akiwa Katibu. Wajumbe wa kamati hii watakuwa ni wawakilishi kutoka sekta mbali mbali katika ngazi za wilaya pamoja na wawakilishi kutoka sekta binafsi, jumuiya za kiraia na za wakulima na wawakilishi kutoka Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, naomba nikumbushe Baraza lako hili tukufu kwamba jukumu la kutekeleza masuala ya uhakika wa chakula na lishe linabebwa na taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama zilivyoainishwa katika kiambatisho namba 1.
Hata hivyo, Wizara ya Kilimo na Maliasili ndio itakayokuwa ni taasisi kuu itakayosimamia kwa karibu utekelezaji wa masuala yote ya uhakika wa chakula na lishe, ikiwa ni pamoja na kuratibu ushiriki wa taasisi nyengine za serikali katika utekelezaji kwa mujibu wa dhamana zao kama zilivyotajwa katika sheria hii.

Katika kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinaelewa na kutekeleza majukumu yao ipasavyo rasimu hii ya sheria imeainisha majukumu ya kiutendaji ya kila taasisi husika ambayo imeainishwa katika kiambatisho namba 2.
Mhe. Spika, mambo mengine muhimu yaliyozingatiwa katika sheria hii ni kama haya yafuatayo:

Uanzishwaji wa Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar *(Zanzibar Food Reserve*).
Mhe. Spika, rasimu ya Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe katika kifungu chake namba 25 (1) imependekeza kuanzishwa kwa Hifadhi ya Chakula Zanzibar ambayo itasimamiwa na taasisi kama itakavyoamuliwa na Baraza la Taifa la Uhakika wa Chakula na Lishe. Madhumuni ya kuanzishwa kwa hifadhi hii ya chakula ni pamoja na haya ninayoyaeleza:

1. Kuhakikisha usambazaji wa uhakika wa chakula Zanzibar.

2. Kukabiliana na upungufu wa chakula unaotokana na majanga kama vile ukame, mafuriko au majanga yoyote yatakayopelekea jamii kukosa chakula kwa nguvu zao wenyewe.

3. Kutoa chakula cha dharura cha msaada *(minimum amount of food)* kwa watu ambao itathibitika kwamba wapo katika hali hatarishi ya kupoteza maisha yao kutokana na upungufu wa chakula, ukame au maradhi kwa mazao yao.

4. Kutatua matatizo yanayokabiliana na usambazaji wa chakula Zanzibar.

Utambuzi wa haki ya kupata chakula *(Right to food).* Mhe. Spika, rasimu ya Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe imezingatia utambuzi wa haki ya chakula na imetajwa katika kifungu namba 20 (1) cha mswada wa sheria hii. Haki ya chakula ilipitishwa na Umoja wa Mataifa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotambua haki hiyo.

Kimsingi, haki ya chakula inasisitiza kwamba chakula ni haki ya kila binadamu. Hivyo basi, makundi hatarishi ya kupatwa na ukame au ukosefu wa chakula yanahitaji yapewe kipaumbele katika kuhakikisha kuwa wana uhakika wa chakula na lishe bora.

Aidha, haki ya chakula pia inazingatia haki sawa kwa kila mwananchi na kusikuwepo na ubaguzi, upendeleo au vikwazo kwa misingi ya jinsia, rika, tofauti ya utamaduni, kabila au imani ya dini, kisiasa au pingamizi nyengine yoyote katika kupata fursa ambazo zitawezesha wananchi kuendeleza maisha yao na kujipatia chakula kwa njia iliyo halali.

Mhe. Spika, nadharia ya haki ya chakula imeainisha dhamana zinazohitaji kuchukuliwa na serikali na wananchi katika kuhakikisha kwamba haki ya chakula inapatikana kwa kila raia wa nchi yetu. Mswada wa Sheria katika kifungu namba 20 (3) umeainisha majukumu na utaratibu wa kufuatwa na serikali ili kutoa fursa na kuweka mazingira mazuri yatakayomuwezesha kila Mzanzibari kwenda kupata haki yake ya chakula kwa kujituma katika njia za haki na sheria na hatimaye kuweza kujikimu kimaisha.

Aidha, mswada pia umeweka bayana jukumu la kila Mzanzibari katika kujihakikishia haki yake ya chakula na lishe inapatikana kwa msingi wa kujituma kwa haki chini ya mazingira mazuri ya kisera na uwezeshwaji yaliyowekwa na serikali. Haya yapo katika kifungu namba 22 cha mswada wa sheria hii.

Adhabu kwa mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza wajibu wake na kujipatia chakula yeye na familia yake kwa kujituma kwa njia za haki nayo imependekezwa na imetajwa katika kifungu namba 23 na 24 cha mswada huu.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika kifungu namba 3 waraka wangu mimi utekelezaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe ni jukumu la wizara mbali mbali kama zilivyotajwa katika kiambatisho namba 1.

Katika kuhakikisha kwamba kila wizara ina uwezo wa kifedha kutekeleza masuala ya uhakika wa chakula na lishe rasimu hii ya sheria inatoa maelekezo ya kuwa kila wizara inatakiwa kuwa na bajeti itakayohusiana na utekelezaji wa

masuala ya uhakika wa chakula na lishe. Bajeti hii iwe ni sehemu ya bajeti ya wizara katika kutekeleza majukumu yake ya kawaida.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar baada ya maelezo ya jumla kuhusu rasimu ya Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya mwaka 2011 na sababu zinazopelekea kufutwa kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 1988 kwa jina maarufu MTAKULA, natumai mmepata wasaa wa kupitia taarifa hii na mtatoa michango yenu adhimu kwa nia ya kuwa na sheria nzuri na iliyotimia ya uhakika wa chakula na lishe katika nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo (Mhe. Salmin Awadh Salmin): Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi rehema kwa kutujaalia uzima, afya na salama iliyotuwezesha kushiriki vyema katika kikao hichi muhimu kinachojadili mustakbali wa nchi yetu na watu wetu.

Aidha, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwanzo wa mswada wa sheria uliowasilishwa hivi punde.

Mhe. Spika, kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipata mashirikiano makubwa wakati wa kuupitia mswada huu kabla ya kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu. Mashirikiano yaliyosaidia kamati ni kupata ufafanuzi wa vifungu mbali mbali vya mswada jambo ambalo limeifanya kazi ya kuupitia mswada huu kuwa rahisi.

Mhe. Spika, niruhusu pia niwapongeze kwa dhati kabisa wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara kwa mashirikiano makubwa wanayotoa mara zote wakati wa shughuli zetu za kazi. Naomba niwataje kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdalla Mohammed Ali	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa	-	Mjumbe
4.	Mhe. Rufai Said Rufai	-	Mjumbe
5.	Mhe. Bikame Yussuf Hamad	-	Mjumbe
6.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
7.	Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	-	Mjumbe

8.	Ndg. Asha Said Mohammed	-	Katibu
9.	Ndg. Amour Moh'd Amour	-	Katibu

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba suala la uhakika wa chakula chenye lishe ni muhimu sana katika taifa lolote duniani. Ukosefu wa chakula cha kutosha ikiwa katika nchi, kijiji, kaya na hata mtu mmoja mmoja ni hatari sana katika jamii yetu. Ndio maana serikali yetu inafanya juhudi za kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata chakula cha kutosha tena chenye lishe.

Mhe. Spika, Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula (MTAKULA) uliobuniwa na serikali yetu miaka 23 iliyopita kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 1988 ulikuwa na lengo linalofanana na sheria hii iliyo mbele yetu. Ijapokuwa yenyewe ilizingatia zaidi kwenye msisitizo wa uzalishaji wa wingi wa chakula na serikali kujiingiza kama mshiriki mkuu tu.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mpango wa Kujitosheleza na Chakula (MTAKULA) ni wa muda mrefu na umepitwa na wakati, pamoja na kwamba uliweza kusaidia wananchi katika enzi zile. Serikali katika juhudi zake za kuhakikisha wananchi wake wanapata chakula cha kutosha tena chenye lishe ikaandaa Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe katika mwaka 2008, sera ambayo haikusisitiza uwepo wa chakula cha kutosha pekee bali ilisisitiza uimarishaji wa biashara na masoko, uwezo wa wananchi wa kima cha chini kimaisha kupata chakula cha kutosha, kupunguza hali tete ya kutokuwa na uhakika wa chakula katika jamii, vile vile kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za ardhini na baharini kwa kuyatunza mazingira yetu.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe ni muendelezo wa utekelezaji wa Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya mwaka 2008. Mswada huu wa sheria unahitaji kuungwa mkono kwani umeweza kuwashirikisha wananchi moja kwa moja wananchi ambao ndio walengwa wenyewe. Lakini pia hata na serikali pamoja na taasisi zake inao mchango kamili wa kushiriki katika utekelezaji wa sheria hii muhimu.

Mhe. Spika, kamati yetu imeridhishwa kamati yetu imeridhishwa kabisa na muundo wa vyombo mbali mbali vitakavyoongoza mpango huu kama vile Baraza la Taifa la Uhakika wa Chakula na Lishe, Sekretarieti yake na uwepo wa Kamati Tendaji. Halikadhalika, zipo pia Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe pamoja na Kamati ya Uongozi ya Wilaya. Mamlaka hizo muundo pamoja na majukumu yake yamefafanuliwa vizuri na yenye kueleweka katika sehemu ya pili ya mswada huu.

Mhe. Spika, kuwa na chakula cha kutosha ni hatua moja lakini kuwa na chakula chenye lishe ni hatua nyengine na muhimu zaidi. Tunaamini kwamba

kilimo cha kisasa chenye kutumia nyenzo za kileo ndicho kitakachotuwezesha kuwa na uzalishaji mkubwa wa chakula pamoja na ardhi ndogo ya kilimo tuliyokuwanayo.

Kwa maana hiyo, tunasisitiza sana kuwa na matumizi bora ya ardhi katika kuziweka mbolea na madawa mengine ya kuulia magugu na wadudu waharibifu.

Mhe. Spika, tusipokuwa waangalifu katika matumizi haya tunaweza kuwa na chakula kingi lakini kisiwe na lishe ya kutosha na pengine kiwe na madhara ya matumizi yake kwa binadamu. Wakati mwengine hata ladha ya chakula chenyewe inapotea. Wengi wanaamini kuwa viazi vitamu vinavyolimwa vikiwa vimewekewa mbolea huwa vinene na vingi lakini ladha yake ni tofauti kabisa na vile visivyolimwa kwa mbolea.

Mhe. Spika, ninachokusudia kusisitiza hapa ni kwamba nyenzo hizi za mbolea na madawa mengine ikiwa ni ya kuulia wadudu au magugu pamoja na mbolea ziwe zinachaguliwa zile zenye kuendana na mazingira yetu. Aidha, watumiaji yaani wakulima wawe na elimu ya kutosha ya kujua kiwango, aina, wakati na pahala pa kutumia nyenzo hizo. Vyenginevyo tunaweza kuwa na uzalishaji mkubwa wa chakula kisichokuwa na lishe.

Mhe. Spika, mswada huu pia umeeleza juu ya wajibu wa serikali na majukumu yake katika kuhakikisha kwamba kuna urahisi wa upatikanaji wa chakula. Aidha, wajibu huo upo pia kwenye kila wizara na vile vile kwa Mkuu wa Kaya. Mhe. Spika, tatizo hapa linaweza likatokea kwenye vigezo vya aina ya chakula chenye kirutubisho. Wasi wasi wetu kusiwe na tafsiri tofauti na sheria hii kwa wanakaya jambo ambalo litazua malalamiko mengi. Kwa maana hiyo basi, Kamati inaiomba wizara itoe taaluma kwa wananchi wetu juu ya hili vyenginevyo wakuu wa kaya siku zote watatinga Mahakamani.

Mhe. Spika, mswada wa sheria hii unapendekeza kuanzishwa kwa Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar. Ni jambo zuri na kwa kweli limechelewa sana kuwepo. Lakini Waswahili wanasema ‘Kawia ufike’. Katika hili Kamati yetu inaiomba wizara mambo yafuatayo:

a) Kuwe na maghala ya kutosha ya kuhifadhia hicho chakula.
b) Usambazaji wa chakula uzingatie uhalisi wa mahitaji ya sehemu husika.
c) Uhifadhi ya chakula uzingatie sana ubora wa chakula chenyewe na masharti ya kiafya.
d) Uhifadhi wa chakula usiwe kwa aina moja tu ya chakula iangaliwe na aina nyengine.

Mhe. Spika, kuwa na uhifadhi wa chakula kunahitaji gharama, hivyo ni vyema serikali ihakikishe kuwa na akiba ya kutosha ya fedha kwa madhumuni hayo. Hali hiyo itauwezesha uhifadhi huo uwe endelevu.
Mhe. Spika, sheria hii itampa waziri kutunga kanuni ambazo zitasaidia utekelezaji wake ili uwe bora. Kanuni hizo zitaangalia sifa na vigezo vilivyo sahihi vya utoaji msaada wa chakula. Taratibu za usimamizi na udhibiti wa hifadhi hiyo ya chakula pamoja na mengineyo yenye kuhusiana na hayo. Kamati inaamini kabisa kanuni hizo zitakazotungwa itakuwa ni zenye kuhifadh haja halisi inayotakiwa.

Mhe. Spika, mwisho kamati yetu anaunga mkono hoja hii, na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni naukubali mswada huu wa sheria nikiwaomba wajumbe wenzangu wauchangie na hatimae waupitishe ili uwe sheria.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kwanza jioni hii ya leo baada ya hotuba nzuri ya Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na afya na kuweza kuzungumza katika Baraza lako tukufu. Pia namshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa jumla kwa kuanza katika kipindi hiki na kuona umuhimu wa kuandaa mswada huu baada ya kupata ile sera ya uhakika wa chakula katika kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, nikitaja neno chakula hakuna ambaye ataweza kubeza umuhimu wake. Kwa hivyo, ni muhimu sana kwamba yale tuliyokusudia katika mswada huu yawe sheria na yawe kweli tumeyakusudia na tutayatekeleza kwa undani na kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kabla sijaanza mchango na kuingia katika mswada wenyewe naomba nitaje mambo ambayo ni muhimu sana katika kufikia sera ya uhakika wa chakula na liche. Mhe. Spika, ardhi yetu ni ndogo, sisi ni visiwa vidogo kwa hivyo, jambo la mwanzo linahitajika kuwe na sera muhimu ya matumizi ya ardhi na kutokana na sera hii ya matumizi ya ardhi, itazuwia ardhi ya kilimo hasa ile yenye rutuba isivamiwe na miradi mingi, kama ujenzi wa miji na mambo mengineyo. Bila ya kuidhibiti ardhi yenyewe, hatutokuwa na mwelekeo wa kupata uhakika wa chakula chenyewe, kwani chakula chote hiki basi kinazalishwa katika nchi, ukiachia mbali kile ambacho kinavuliwa baharini.

Pili Mhe. Spika, na bahati nzuri wizara hii vile vile imepewa maliasili, ni vizuri kuhifadhi misitu ili kuweza kupata mvua za kutosha. Kwa sababu kilimo chetu sana kinategemea upatikanaji wa mvua, ili kuelekea katika uhifadhi, uhakika wa upatikanaji wa chakula, basi tunapaswa sana kuhifadhi misitu yetu. Lakini sio misitu peke yake na miti ya chakula.

Mhe. Spika, kwa hii misumeno iliyoingia sasa hivi, miti inakwenda sana. Kuna msumeno unaojulikana sana kama ni *canso*. Sasa kwa *speed* inayokwenda ya miti na kwa bahati mbaya miti mingine ni ya matunda. Mhe. Spika, kuna neno linaitwa ku-*subsidization*, kwa maana ikiwa mwananchi atapata shelisheli lake, ile pesa ndogo anayoipata basi atakwenda kununua dagaa, kwa hivyo keshafanya urutubishaji wa lishe. Lakini ukiukata mshelisheli na ikawa shelisheli halipo. Kama tulivyopewa juzi takwimu katika semina, na namshukuru Mhe. Waziri kwamba watu wengi, hata wa vijijini wanategemea sehemu kubwa ya chakula chao kununua. Sasa hapo ikiwa miti ya matunda itaendelea kukatwa, basi ile *subside* ya fedha anayopata yule mwananchi badala ya kwenda kununua samaki au dagaa akapata lishe bora basi ataendelea kununua *starch*. Kwa hivyo, utunzaji wa miti ya matunda ni muhimu sana katika kuelekea uhakika wa chakula.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo litatupelekea kupata uhakika wa chakula ni kuweka mkazo juu ya kilimo cha kutumia *machine*, yaani *make a nice the family*. Hali inayokwenda sasa hivi kama tunavyopewa takwimu ni kwamba ekari kubwa inalimiwa kwa mikono kuliko kwa *machine* au kwa matrekta. Tunaiomba sana Wizara ya Kilimo na Maliasili ikishirikiana na Serikali Kuu, ili kuhakikisha kwamba tunafanya mabadiliko makubwa katika kilimo chetu cha kuelekea katika utumiaji mkubwa zaidi wa *machine* au matrekta.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo lingeweza kutuhakikishia uhakika wa chakula, ni utaalamu wa kuongeza uzalishaji kwa hekta moja. Hivi sasa wazee wetu ndugu zetu wanaolima mpunga wanajitahidi sana, lakini pato lao ni dogo sana ukilinganisha na ile kazi ambayo wanafanya. Kwa hivyo, ikiwa kuna utaalamu wowote, ambao ikiwa ni kwa njia ya kumwagilia maji au kwa njia ambayo ni ya kupata mbegu ambazo zinazalisha zaidi, lakini ni kuhakikisha kwamba tunazalisha zaidi katika ekari moja au hekta moja basi ni suala muhimu sana kuliko kubaki katika ukulima huu huu, ambapo akimaliza shamba na mpunga wake umeshamaliza kabakisha wa mbegu tu.

Mhe. Spika, kwa sababu ukulima mwingi umeelekezwa katika kuzalisha vyakula vyenye *starch*, vile vile tuna budi kupeleka nguvu zetu katika kulima mazao ambayo yataweza kutupatia *protein* na vitamin, ambavyo ni vyakula vya kunde, uvuvi wa baharini pamoja na ukulima wa mboga ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwenye utangulizi wa namna gani tubadilike katika kilimo chetu. Naomba sasa Mhe. Spika, kwa ruhusa yako niingie kwenye mswada wenyewe ambao utapelekea kupatikana kwa vyombo mbali mbali vya kutimiza malengo ya mswada huu.

Mhe. Spika, naanzia na Muundo wa Baraza la Uhakika wa Chakula, katika ukurasa wa 104. Mhe. Spika, mimi sina tatizo na muundo, isipokuwa kifungu cha (c). Kwa maoni yangu naona jadwali la kiambatanisho nambari 1 ni kubwa mno. Kwa sababu kikawaida mfanyakazi yeyote akianza ngazi ya Katibu Mkuu, anapochaguliwa kuwa yeye ni Katibu Mkuu wa Wizara, basi anakuwa ndio mtekelezaji mkuu wa shughuli za serikali zilizoelekezwa kwake, ikiwa ni za wizara yake au zinahusiana na wizara yake, lakini zinatokana na sekta mbali mbali.

Sasa Mhe. Spika, chombo hiki ukiwawekea wote hawa 16, kwa kweli ni wengi sana, wengine wote ni watu ambao ni wa kupokea tu, lakini ingefanyika hivi kwamba wale ambao wanaingia moja kwa moja katika uzalishaji wa chakula au ufuatiliaji wa lishe, ndio ambao wangehusika na kupanga hizo sera. Mimi nimetaja tano tu hapa, katika 16 nimetaja tano tu, nyengine zote naona ni watu ambao wangekaa wakasubiri wanapangiwa nini ili wakatekeleza.

Kwa mfano, wizara husika na mifugo, wizara husika na uvuvi, wizara husika na biashara, wizara husika na tawala za mikoa na wizara husika afya. Ndio wizara ambazo moja kwa moja ukiikamilisha na hiyo wizara yenyewe ya kilimo na maliasili ndio moja kwa moja wanahusika na uzalishaji wa chakula pamoja na ufuatiliaji wa lishe.

Mhe. Spika, sasa tukiweka timu kubwa maana yake kutakuwa na urasimu mwingi wa kungojana, vikao vinaweza vikachukua muda mrefu kwa sababu huyu yupo huku na huyu kasafiri au wengine wamekwenda na Rais huku, ili kupata ule ufanisi wa hili Baraza basi tuchukue sehemu ndogo tu ya makatibu wakuu tuwaweke, ili wengine sasa watafuata kutekeleza yale ambayo yameamuliwa. Hilo la mwanzo katika huu mswada wetu.

Halafu jambo la pili, Mhe. Spika, ambalo nitaunganisha kifungu cha 6 na kifungu cha 25, kinachozungumzia kuhusu hifadhi ya chakula. Kifungu cha 6(e) naomba ninukuu, kinasema;

Kifungu cha 6(e)

> "moja katika kazi hilo Baraza kuamua kwa niaba ya serikali juu ya hali ya hatari inayoleta kutolewa akiba ya chakula ya Zanzibar na kwa kiwango maalum".

Hapa mimi nazungumzia kuhusu akiba ya chakula. Vielelezo vya wataalamu kutoka *FAO* wametoa mambo matatu ambayo ndio yanayoweza kutumiwa kwa kuweka na kutoa akiba ya chakula.

Jambo la mwanzo ni hili lililotajwa hapa, dharura ya upatikanaji wa chakula ikitokezea. Lakini la pili ambalo linatokezea kila mwaka katika nchi yetu, huu mswada haujalizungumza, ni kusawazisha bei.

Mhe. Spika, tumeona kwamba kila mwaka sasa hivi ikifika kipindi fulani vyakula sio kwamba havipo, lakini vinapanda bei sana. Sasa wataalamu wanasema kwamba ni wakati huu ile ghala ya akiba ndipo inapotumika kwa ajili ya kutoka katika soko sasa, yaani limeingia katika soko ili kuiweka ile bei iwe kama ilivyokuwa au kama itapanda basi ni kidogo sana.

Kwa hivyo, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba je madhumuni mamoja ya hii hifadhi ya akiba ya chakula, hii ya kutuliza bei wakati wa mfumuko wa bei unapotokea, itajumuishwa katika shughuli hii au bado kwanza ni mapema. Ikiwa halikuzungumzwa basi mimi naomba sana kwamba moja kati ya tatizo letu kubwa linalojitokeza kila mwaka ni kupanda kwa bei ya vyakula kwa ghafla. Hii hifadhi ya akiba ya chakula ndipo inapotarajiwa sasa iingie katika soko ili bei ziweze kutulia na wananchi waendelee na maisha yao kama ambavyo walikuwa wakienda. Hilo ni suala la pili.

Mhe. Spika, suala la tatu ambalo nataka kulizungumza ni kwamba nina wasi wasi kuwa kumechupizwa katika huu mswada. Mhe. Spika, katika kifungu cha 8 na cha 9 kinazungumzia kuhusu sekreterieti ya Baraza lenyewe. Lakini kifungu cha 10 na cha 11 kinazungumzia kuhusu kamati tendaji, ambapo kwenye mswada wa Kiingereza imeitwa *steering committee*. Sasa kwa mujibu wa vifungu hivi, utaona kwamba hii kamati tendaji ni kubwa zaidi kuliko ile sekretarieti. Sasa hivi vifungu hivi sekretarieti inakuja mwanzo halafu ndio ije kamati tendaji katika mpangilio wa huu mswada.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria unaruhusu basi hamna matatizo, lakini inaonesha kwamba sekretarieti ni chombo kidogo kuliko kamati tendaji au *steering committee* kama ilivyotajwa katika mswada wa Kiingereza. Kwa hivyo, naomba hapa na Mhe. Waziri apatizame ikiwa sheria inaruhusu chombo kidogo kutajwa mwanzo halafu ndio kije kile kikubwa, laa hairuhusu basi naomba pafanyiwe marekebisho ili ule mtiririko wa kutoka Baraza la Uhakika wa Chakula halafu chini yake inakuja kamati tendaji, chini yake ndio panakuja maelezo ya sekretarieti.

Mhe. Spika, lakini katika mnasaba wa kifungu cha 10 kuanzishwa kwa kamati tendaji, narudia tena ile hoja yanagu ambayo niliitoa katika muundo wa Baraza. Mhe. Spika, kifungu cha 10(b) cha mswada huu kinaeleza kwamba wajumbe watakaokuwa katika kamati tendaji ni makatibu wakuu wa wizara husika. Kwa hivyo, narudia kusema kwamba hata hii kamati tendaji tena, kwa mujibu wa maana ya wahusika ni ile ile jadwali ya mwanzo, kwa hivyo narudia kusema kwamba ni jadwali kubwa sana. Napendekeza hapa kwamba bado wapunguzwe, badala ya 16 tunawafanya watano tu na wa 6 anakuwa ni yule wa kilimo mwenyewe.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe muda.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, suala la mwisho kabisa nije kwenye kifungu cha 13. Kifungu hiki kinasema kuanzishwa idara katika wizara ambayo itajulikana kama idara ya uhakika wa chakula na lishe, hicho ndio ninachozungumza.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 13(2) kinasema, idara itakuwa na Mkurugenzi ambaye atakuwa na jukumu la kuratibu shughuli za kila siku za kiidara. Pia wafanyaka wengine kama itakavyoamuliwa na Mkurugenzi. Hapa inaonekana kuwa sekreterieti iwe imekwisha. Lakini kuna kitu chengine hapa kimeingia cha 3 na 4. Idara itakuwa na Afisa maalum kutoka kila wizara husika na wilaya ambao watateuliwa na katibu mkuu wa wizara husika na mkuu wa wilaya husika. Afisa Maalum atakuwa na jukumu la kuwezesha na kusimamia shughuli za uhakika wa chakula na lishe ndani ya eneo la wilaya husika.

Sasa vifungu hivi viwili vya 13 na 14 sioni umuhimu wake. Kwa sababu kutokana na teknolojia iliopo Mhe. Spika, kwa mawasiliano, unaweza ukafanya mkutano sasa hivi baada ya dakika tano wizara zote zikapata taarifa kwa kupitia mtandao nini kimezungumzwa. Sasa ya nini kuwaita watu tena na kurudi nyuma katika ile wakati ambao kupeana habari ni kwa njia yam domo. Kwa hivyo, naona mkumbo wote wa watu huu hauna hauna haja tena. Idara wenyewe njia ya kupeana habari iwe ni kwa njia ya matandao na kwa njia ya kama kutoa *photocopy* na njia nyengine. Kwa hivyo, bado tuna njia ya kupunguza urasimu na kupunguza msururu mkubwa wa watendaji katika shughuli nzima ya kufuatilia suala hili.

Nakushukuru sana Mhe. Spika. Mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Ziwani, naunga mkono kwa dhati sana mswada huu wa kutuhakikishia upatikanaji wa uhakika wa chakula, kwani ni jambo ambalo lina umuhimu wa pekee katika maisha ya binaadamu, ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia katika mswada huu wa chakula na lishe wa akiba ya nchi yetu. Mhe. Spika, kazi hii tumekwishaifanya kwa ufanisi mkubwa sana tukiwa ndani ya kamati, kama vile Mwenyekiti wetu wa kamati alikwishaelezea. Isipokuwa mimi nina angalizo.

Mhe. Spika, wakati wa ufuatiliaji wa baadhi ya mambo ndani ya wafanyakazi wa wizara husika, hususan kwa wale mabwana shamba. Wao walikuwa wana angalizo la kuomba kwamba vile viwango vya fedha kwa ajili ya kufanikisha suala hili, wanaomba sana kwamba viwe vinakwenda kwa wakati. Kwa kupitia Baraza lako la Wawakilishi hili, tunaomba zile fedha zinazokwenda kwa sababu ya kufanikisha mpango huu, ziende kwa wakati, kwani programu ya kilimo inakwendana na masuala ya mvua na mambo mengine. Sasa kama mvua itakuwa imepita, ule msaada wa kifedha ukaja baadae basi yale malengo hasa yatakuwa hayafikiwi.

Kwa hivyo, mabwana shamba hawa pamoja na wakulima walikuwa wana maombi maalum kwamba hizi fedha kwa sababu ya kufanikisha suala hili zije kwa wakati ili waweze kufikia kile kiwango cha uzalishaji ambacho wao wenyewe watakuwa wamekilenga.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu ulikuwa ni huo, kwa sababu maeneo yote tumeshatembea, tunashukuru kwamba mswada huu uko safi, wizara pamoja na waziri wamefanyakazi nzuri. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kikwajuni, naunga mkono hoja ahsanteni sana.

Mhe. Assaa Othman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema, tukakutana tena na kuweza kuendelea na shughuli hizi tulizokabidhiwa na wananchi wa nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri mwenye zamana ya wizara hii kwa kuona umuhimu wa mswada huu ni kweli kabisa umekuja wakati muafaka, tukitilia maanani kwamba ulimwengu wa sasa hivi unakabiliwa na hali mbaya ya mapungufu ya chakula.

Mhe. Spika, pia dunia inakabiliwa na mtikisiko ya mabadiliko ya utabia nchi, tunayaona hayo kwa wenzetu, lakini na hata sisi tunapata madhara ya zile cheche, Mwenyezi Mungu aendelee kutunusuru na hayo makubwa.

Mhe. Spika, nilianze kusema kwamba mswada huu umekuja wakati ndio, lakini kukumbuka hilo ni vyema tufahamu kwamba tuna deni kubwa kama taifa lile la azimio la Maputo linalotutaka angalau asilimia 10 ya bajeti ya wizara hii ya

taifa iwepo, ili waweze kuendeleza yale ambayo tunayasema sisi na yale wanayojipangia wenyewe, hatuna budi tuisukume basi bajeti ya serikali kwa wenzetu hawa ili waweze kumudu haya waliojipangia.

Mhe. Spika, mswada una nia ya kujenga misingi ya kisheria juu ya utekelezaji wa sera ya uwahakika wa chakula na lishe, ambayo tayari tumeshakuwa nayo, lakini sasa suala la utekelezaji na kuwa na ufahamu na wajibu wa jambo hili ndio sasa nadhani tumefika wakati muafaka.

Mhe. Spika, suala la miundo ya Baraza la Taifa, kamati tendaji na idara zake hizo, nashukuru kwamba Mhe. Maalim Rashid amelitolea maelezo, nadhani sina haja ya kurudia tena huko. Lakini nataka niseme kwamba wizara husika na kama nia njema iliyoonyeshwa na serikali kutenga Wizara ya Mifugo na Uvuvi peke yake ni jambo zuri na katika suala hili wizara mbili hizi hazina budi zishikamane kabisa, kwa sababu moja itatoa chakula na nyengine itatoa kitoweo ndio tunapopata lishe. Kwa mashirikiano hayo hayo tutaweza kupata mbolea ya kuzalisha hayo mazao.

Kabla ya kutizama ghala, Mhe. Spika, kwanza kuna kazi ya kujenga huo ufahamu. Kumeorodheshwa wizara kadhaa huku, naiona Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto ipo, vijana na suala la kilimo kidogo watakuwa mbali mbali. Sasa ni kazi ya wizara hurika kujenga ufahamu wa vijana hawa ambao sasa hivi wameshasalitika mno kwa bangi na madawa ya kulevya, tuwaondowe huko.

Wizara ya Afya pia ina kazi hiyo ya kuwalea mpaka tufike nao hapa ili waweze kukifahamu kilimo na tija yake.

Mhe. Spika, kazi hiyo haitokuwa ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Lakini takriban ni wizara zote kwa namna moja au nyengine kila mmoja kwa upande wake, kwamba tutalazimika kufanyakazi hii kwa ajili ya kuhakikisha kuwa taifa hili linaondokana na njaa, hakuna Mzanzibari anayekula mlo mmoja na pia hakuna Mzanzibari anayekwenda kwa Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni Haji kwa kukosa damu.

Kwa hivyo, kazi hiyo hataiweza ndugu yangu Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid ni lazima Waheshimiwa Mawaziri kwa upande wao kila mmoja aweze kuwajibika kwa namna itakavyowezekana.

Mhe. Spika, katika hali hiyo hatuwezi kulidharau kamwe wala kubeza suala la mazingira. Kwa hivyo, tutaendelea kusema kupiga makelele, lakini ule ufahamu na utekelezaji kila mmoja kwa nafasi yake.

Mhe. Spika, suala la mazingira ya ardhini na baharini ni tishio, Zanzibar ni kisiwa kidogo, idadi ya watu inakua, mahitaji yanaongezeka, *technology* ya ulimwengu inakua, vijana tunaowazaa sasa wanahitaji kuja kuikuta Zanzibar nzuri.

Lakini nathubutu kusema tena nasikitika sana tuliopo tunaiacha Zanzibar inapopotolewa na wenzetu wachache sana kwa tamaa zao, mazingira yanachafuliwa vibaya sana na kila eneo yupo kiongozi. Kwa mfano, yupo Sheha, Diwani, Mwakilishi, Waziri pamoja na wengineo, sasa yanayotendeka humo wanayashuhudia kwa macho yao, lakini bado hakuna hatua yoyote inayoendelea. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mazingira haya kama tutaendelea kuyaacha hivi yalivyo sasa, basi mswada huu utabaki kwenye karatasi, lakini *implementation* yake iliyokusudiwa nasikitika kusema kwamba sidhani kama tutaikuta hata kidogo.

Kwa kweli mazingira yetu ni muhimu tuyatunze tena tuyatunze kwa nguvu moja, yaani kila mmoja wetu afahamu kwamba anao wajibu wa kutunza mazingira yeye mwenyewe na eneo ambalo anaishi. *(Makofi).*

Mhe. Spika, maeneo ya kilimo ndio yanayoharibiwa kwa kujengwa nyumba za makaazi. Vile vile vianzio vya maji ambavyo tunavitegemea katika shughuli nzima hii vinavurugwa, lakini wanaotoa vile vibali vya ujenzi ni hawa ambao tuliomo humu ndani na hali hii inasikitisha sana.

Kwa maana hiyo, tunasema nini na tunachokifanya ni kipi. Kwa hivyo, neno ufahamu na utekelezwaji wa hilo tutakalolifahamu lazima yaende sambamba.

Miti na nilikuwa nikimuomba sana Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid wakati alipokuwa na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, kwamba katika masharti ya kutoa viwanja, basi moja wapo iwe ni kupanda miti kwenye kiwanja kile angalu miti minne, yaani kila pembe kuwe na mti mmoja. Kwa hivyo, nadhani hali hii ingesaidia kuona kwamba miti kumbe ina umuhimu wa aina yake.

Mhe. Spika, hata kwenye mji wetu kuna maeneo ya wazi ambayo yanastahiki kuwe na miti na wataalamu wapo wa kuelekeza hilo. Kwa mfano, hivi sasa mvua zimepungua kwa kiwango kikubwa na tunaendelea kulalamika na mvua zitaendelea kupungua sana kutokana na hali inayoendelezwa sasa.

Kwa kweli Zanzibar baada ya miaka kumi na tano ijayo itakuwa hatari kubwa. Kwa mfano, mazao ya kilimo yanahitaji maji, sasa tutayatoa wapi na wala hatuna mvua, lakini hayo yaliopo na yale tunayoyapata siku ile mvua

inaponyesha tunayahifadhi vipi. Kwa hivyo, ni vyema tuwe na utaratibu unaotoa sura kwamba kweli ile dhana ya *water harvesting* itakuwa inatekelezeka.

Kwa maana hiyo, tujipange kuweza kutekeleza hili, kwa sababu mvua inanyesha na maji yote yanamalizikia baharini na inapopita miezi mitatu tunalia ukame kwani mazao haya hatuna vyakuyafanya. Kwa mfano, hivi sasa migomba kadhaa imeharibika, michungwa imenyauka pamoja na mazao mengine mengi.

Kutokana na mazingira hayo, wakulima wetu wako katika hali ngumu sana ya uzalishaji. Kwa kweli wanajitahidi lakini matokeo yake hakuna *support* inayowafanya wao waweze kuendelea kuzalisha, yaani kila wanachokizalisha hakuwasaidii wao na wala wenzao, maana yake kinafika soko bila ya kuwa na hadhi kwamba sasa ni tayari zao la kula binadamu na kuweza kupata hiyo lishe iliyokusudiwa.

Kwa hivyo, hapa taasisi hizi zilizoorodheshwa hapa nasema kwamba kila moja itakapowajibika ipasavyo, kumuwezesha huyu mkulima kwanza kumudu kuzalisha. Mhe. Spika, pembejeo zinahitajika ili aweze kuzalisha na hizo ni ghali mno na watu wetu ni masikini sana na wanahitaji msaada maalum, ili waweze kuzalisha mazao yao.

Vile vile hatuwezi kuliacha hili baada ya kuzalisha kuhusu masuala ya miundombinu na Waziri Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Hamad Masoud Hamad, kwa kweli yeye anamchango wa pekee kumuwezesha mkulima huyu baada ya kuzalisha alitoe zao hilo shambani na kufika alikokusudia.

Mhe. Spika, wakulima wanabeba mazao yao vichwani, mabegani na kupeleta barabarani kwa ajili ya kusubiri usafiri wa gari, yaani sehemu inayofika gari. Kwa kweli maeneo mengi na hususan Kisiwa cha Pemba kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Said Ali Mbarouk, kule nilikozaliwa mimi Mtambwe mazao yanaharibika na wala hakuna usafiri wa kuyafikisha sokoni.

Kwa hivyo, matokeo yake hawezi kufaidika na kile anachokizalisha na yeye anahitaji alipe mahitaji ya skuli, pia anahitaji kumsaidia mama wakati anapokwenda hospitali na hata mahitaji yake mwenyewe ya kifamilia, kitu cha kuuza na kupata hayo yapo lakini kuyafikisha kunakokusika ni soko na wala hana uwezo huo. Suala la miundombinu si kwenda kupiga kiparapara wakati wa kununua karafuu, isipokuwa ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na miundombinu ya uhakika ya kuwawezesha wakulima kusafirisha mazao yao.

Mhe. Spika, suala la miundombinu likikaa mahala pake, lakini mabenki yetu kuna haja ya kutoa huduma ya kuwakopesha ya wakulima wetu waweze kumudu kununua pembejeo, mbegu bora za kupandia. Kwa kweli hivi sasa kuna wajanja ambao wanatoa mbegu kwa namna wanavyofahamu wao, sasa wakulima wetu taaluma ya kujua hii ndio au sio hawana na matokeo wananunua mbegu ambazo si nzuri na hasara ni mara mbili, yaani anakosa chakula chake pamoja na mtaji aliokuwa nao.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kazi hii ya wizara yako mwenywe na jambo la msingi ni wataalamu wetu kutoa taaluma kwa wakulima wetu, ambayo ni bora zaidi kwa lengo la kuwa na ufahamu mzuri. Kwa maana hiyo, zile Skuli za Wakulima ziendelezwe na ziwe imara zaidi kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la usafiri wa mazao haya yakeshakupatikana. Wakulima wetu wanasafirisha mazao yao, lakini njia ni mbaya sana na wala haifai. Kwa mfano, anatoa mikungu 100 Mkoani Pemba na kufika nayo Bandarini Unguja 40 na iliyobakia 60 yote imeshavurugika.

Kwa kweli utaratibu ule wa kurundika ndani ya meli bado hatujawatendea haki kabisa kusema kilimo hicho tunachokisema leo kiwe bora na lishe iwe nzuri nadhani bado. Vile vile hata samaki hivi sasa wanatolewa Pemba wanaletwa hapa, lakini wanapoletwa wengi wao wameshaharibika.
Sasa haya mambo Mhe. Spika yanahitaji kwanza yafanyiwe utaratibu mzuri wa kuhakikishiwa kwamba wavuvi wanawezeshwa kuvua mazao ya baharini, yaani samaki hawa wanakuwa vipi kufika walikokusudiwa, pia na mazao kama vile ndizi na matunda pamoja na mengineyo yanafika kule yalikokusudiwa yakiwa na tija ya kumuwezesha mkulima kupata malengo aliyokusudia.

Mhe. Spika, suala la uvuvi nalo lina namna yake na hivi sasa linaingiliwa na uvuvi haramu. Kwa kweli hapa lazima tujipange ili kuwawezesha wavuvi wetu kuweza kuvua na kupata ile riziki yako halali bila ya kuchafua mazingira.

Kwa maana hiyo, taaluma inahitajika lakini kuondoa malalamiko ni kueleweshwa wakafahamu, lakini baada ya kufahamu mbadala naendelea kusema kwamba hawa ni masikini, basi tutafute utaratibu wa kuwawezesha wasiharibu mazingira sambamba na hilo kazi yao waendeleze ili tuweze kuishi.

Mhe. Spika, maji ni uhai narudi tena katika suala la maji. Mabadiliko ya tabia ya nchi hivi sasa ni tatizo la dunia. Kwa kweli kuna haja ya kuyatunza vizuri, yaani vyanzo vyetu vya maji ni lazima tuvitunze na kila mmoja awajibike kwa hili.

Hivi sasa maji mengi yanapotea na vyanzo vingi vinakauka na wala sitaki niseme kwamba ni uzembe au vipi, lakini ninachoweza kusema ni kwamba bado hatujawajibika ipasavyo, kwa sababu haya yanatendeka mbele ya macho yetu na tunashuhudia.

Lakini mazao ya mboga mboga na matunda kwa ufinyu wa ardhi iliopo Zanzibar, basi huu ni ukombozi tosha kwa wakulima wetu wa vijijini, ikiwa tutawajengea mazingira bora, basi wataweza kutumia maji na kuzalisha mboga mboga na matunda na kupata Viwanda Vidogo Vidogo na Vyakati na kuweza kuendesha maisha yao pamoja na familia zao.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache sana naomba kuunga mkono hoja hii mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wete Kisiwani Pemba. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi kwanza nitoe shukurani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii, kwa ajili ya kutoa mchango wangu mdogo wa mawazo katika mswada huu uliowasilishwa na Mhe. Waziri asubuhi ya leo.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika mswada huu ambao unafuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula Nam. 3 ya mwaka 1988 kuweza kutunga Sheria Mpya ya Chakula na Lishe Zanzibar na mambo mengine yanayofanana na haya.

Kwa kweli tunashukuru Baraza lako tukufu limepitisha Sera pamoja na Sheria mbali mbali za kuhakikisha kwamba tunakuwa na uhakika wa chakula. Lakini mara nyingi tumekuwa tukipitisha sera na baadaye tunaunda sheria na tatizo letu kubwa linakuwa katika usimamizi na utekelezaji wa hizi sheria zetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi sasa tumepata makabrasha ambayo kuna Rasimu ya Sera ya Kukabiliana na Maafa ambapo kesho tutapata semina. Tukiangalia rasimu hii ya Sera ya Kukabiliana na Maafa, basi kuna mambo moja kwa moja yamegusa mswada huu wa leo. Kwa hivyo, mswada huu ambao aliouwasilisha Mhe. Waziri ni muhimu sana kwa taifa letu pamoja na uhakika wa wananchi wetu.

Kwa kuanzia mchango niende katika suala la maji, kwa kweli hatuwezi kuzungumzia kilimo bila ya kuwa na uhakika wa maji. Mhe. Spika, tunayo Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2004, tukiangalia katika sera ile kuna maelezo mengi ambayo ni mazuri, ambapo kama tutaweza kuitekeleza vizuri, basi kwa kiasi fulani nchi yetu ya Zanzibar, yaani Visiwa vya Unguja na Pemba Mwenyezi Mungu amevijaalia baraka kubwa sana ya maji.

Lakini kutokana na kwamba tunatunga sera na sheria, sasa katika usimamizi na ufuatiliaji tunakuwa hatushughuliki na matokezeo yake yale maeneo ambayo yamezungumzwa katika sera na sheria kwamba yatunzwe kwa ajili ya upatikanaji wa maji, basi maeneo yale tunayaharibu kwa makusudi kama alivyosema Mhe. Asaa Othman Hamad.

Kwa kweli uharibifu wa mazingira umo ndani ya majimbo yetu na sisi wenyewe Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo 50, Viti Maalum pamoja wale Walioteuliwa na Mhe. Rais tunaona na tunashuhudia lakini hakuna hata mtu mmoja ambaye anayeweza kukemea uharibifu wa vyanzo vya maji.

Mhe. Spika, ndipo pale niliposema kwamba tunatunga sheria na sera nzuri tena nyingi, lakini katika utekelezaji hakuna mtu anayewajibika katika utekelezaji pamoja na usimamizi wa maeneo hayo.

Hivi karibuni tumeshuhudia katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi kuna wananchi wetu walikuwa wakipata chakula cha kujitosheleza mwaka mzima kwa kulima mazao yao ikiwemo mpunga, migomba na na mazao mengine ya matunda.

Mhe. Spika, hivi sasa maeneo yale ndio yamekuwa makaazi ya watu, pia kwenye vianzio vya maji watu ndio wamekwenda kujenga, kwa sababu kuna vitu viko *practical* na wala hakuna haja ya kusadikika kama vile ukatolewa mfano wa Ulaya, yaani hapa Zanzibar katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa mfano, kuna maeneo yalikuwa ni chemchem ya maji na hivi sasa pale ambapo palikuwa na chemchem ya maji unalikuta kontena la nyumba limewekwa na wala maji yakuna.

Kwa hivyo, wale watu waliokuwa wakitegemea chemchem ile, hivi sasa wako Darajani kila Ijumaa nafikiri leo waliopita wamewakuta nje ya misikini wanaomba omba. Sasa ndipo pale ninaposema kwamba tunatunga sera pamoja na sheria nzuri tu, lakini kwa kuwa hatuwezi kuzisimamia matokezeo yake omba omba wanaongezeka katika nchi yetu. Kwa kweli mswada huu ni mzuri, lakini bado narudi katika utekelezaji.

Mhe. Spika, naomba kutoa mfano mwengine katika eneo la Upenja au Pangeni hivi juzi nilipita nikakuta kuna *Tsunami* ya minazi na miembe pamoja na miti mingine mbali mbali, basi niliuliza je hapa ulipita upepo, lakini nilipoangalia pale nadhani aidha shoka au misumeno ya umeme umegharikisha mashamba katika eneo lile.

Nimesikia kuna tajiri mmoja amenunua mashamba ya watu tofauti na maeneo wananchi walikuwa wakilima mazao ya kilimo, kwa ajili ya kupata chakula, sasa kwa taarifa nilizozisikia anataka kupanda *spices*.

Sasa ninajiuliza ardhi hii haina mwenyewe, kwa sababu wakati mwengine wananchi wetu tunapowaachia tu na jana tumepitisha Sheria ya Kurasimisha Rasilimali za Wananchi, kwamba ile rasilimali uliyokuwa nayo uweze kupata hatimiliki na kuweza kwenda kuikopea.

Kwa hivyo, kabla ya ile sheria haijapishwa ya kurasimisha rasilimali ya wananchi hivyo vikataa walivyokuwa nayo na sio kama wamekwenda kukopea benki, yaani tayari wameshaviuza na hapo njaa inaanza.

Kutokana na hali hiyo, naiomba Wizara ya Kilimo na Mifugo kupitia kwako Mhe. Spika, kwa sababu ndio zaidi inayoshughulikia masuala ya uhakika wa chakula ijaribu kufuatilia. Kwa kweli kwa taarifa nilizonazo tajiri yule bado anaendelea kuwatafuta wenye mashamba wengine, kwa ajili ya kuendelea kuyanunua na kukata hiyo miembe pamoja na mazao mengine yaliyokuwemo kwa lengo la kupanda *spices*, kwa kujitosheleza yeye mwenyewe.

Mhe. Spika, kama hatukuwa na tahadhari na serikali kama haikuchukua mamlaka yake, kwa sababu pamoja na kwamba ni mashamba ya wananchi, lakini inapofika pahala ardhi ya kilimo inatumika kwa matumizi mengine ambayo hayatusaidii kwa chakula. Kwa hiyo, *spices* ndio watakuja watalii na kununua kama vile hiliki na mambo mengine, lakini njaa tayari imeanza pale, kwa sababu yale maeneo ya kulima chakula tayari yanaanza kulimwa *spices*.

Sasa lazima tuwe na utaratibu, yaani kuwe na maeneo ya kushughulikiwa masuala ya *spices* na yale maeneo ambayo ni ardhi ya kilimo, basi ni vizuri serikali ikawa hata kama eneo lako ni vyema serikali iwe na mkono wake kusema kuwa pamoja na kwamba hili ni eneo lako. Lakini kwa matumizi ambayo unatakakuyafanya na yatapunguza lishe katika nchi yetu, basi serikali ni vizuri kuwa na mkono wake kwa ajili ya kudhibiti. Vyenginevyo tajiri yule anaweza kununua mpaka akafika Mkoa wa Mjini Magharibi na kupanda *spices* mote humu na hali sijui itakuwa vipi.

Kwa kweli katika mazingira kama hayo, hata Mhe. Waziri akijenga ghala basi sijui liwe na ukubwa gani, maana yake huko njaa itakuwa tayari na watu kazi yao itakuwa ni kupanga foleni huyu ngapi na yule ngapi.

Mhe. Spika, nadhani hifadhi pamoja na uhakika wa chakula masuala ya ghala yawe ya mwisho kabisa, lakini kuhakikisha kwamba kila ardhi ambayo tunaweza kuitumia kwa kilimo basi tuweze kuitumia vizuri.

Nikiendelea na mchango wangu katika mswada huu imeelezwa kwamba kuna wizara tofauti ambazo zinawajibika katika kusimamia masuala mazima ya uhakika wa chakula. Kwa hiyo, nashukuru na ndio maana nikasema kwamba suala hili sio la Wizara ya Kilimo peke yake, isipokuwa kila wizara inatakiwa isimamie majukumu yake.

Kwa mfano, kama Tawala za Mikoa Mhe. Spika, maeneo yote ambayo yanajengwa, basi Tawala za Mikoa kwa njia moja au nyengine itakuwa yanahusika katika utoaji wa vibali kupitia kwa masheka na wadiwani pamoja na kwamba kumepatikana baraka kutoka katika Idara inayoshughulikia masuala ya Ardhi. Kwa hivyo, kuhakikisha kwamba yale maeneo ya uzalishaji tunayalinda ili wananchi wetu wawe na uhakika wa chakula.

Mhe. Spika, hivi karibuni ulipotutuma tufanyekazi za kamati. Kwa kweli tulitembelea maeneo mbali mbali ya Kisiwa cha Pemba, kuna maeneo ambayo hivi sasa tumegundua kuwa serikali kama haikuwa makini na kutumia mkono wake kuzuia uharibifu wa mazingira, basi kuna hatari baada ya miaka ya hivi karibuni maeneo yale watu wakashindwa kupata maeneo ya kilimo.

Kwa mfano, katika maeneo ya Mwambe, yaani Vitongoji ndani, kwa kweli tuliwakuta watu wanakata matofali ya mwamba, basi tulijaribu kuuliza haya maeneo mnayapata kwa njia gani. Mhe. Spika, wengine walituambia kwamba wananunua kipande cha shamba la mtu wengine wanauziwa shilingi 300,000/- au 400,000/-.

Sasa ukiangalia lile eneo ambalo ameuziwa yule mkataji wa matofali, basi eneo lile kuna mazao ambayo yalipandwa, kwa hiyo mazao yale mwananchi alikuwa akiyatumia pamoja na familia yake kwa ajili ya kupata chakula. Kwa hivyo, maeneo yale hivi sasa ile ardhi ya juu inasombwa na watu wanautafuta mwamba chini wanakwenda na misumeno yao kwa ajili ya kukata mafotali.

Kutokana na hali hiyo, sisi tulijiuliza ardhi ile hata wazee wao mpaka wao wakafikia pahala kuwa na nguvu za kuwa na misumeno ya kupasulia hiyo miamba, wazee wao katika maeneo yale walikuwa wakilima na ndipo wao wakakua na kuwa na nguvu zile. Sasa kama wazee wao kama wangelichimba mahandaki yale hicho chakula cha kuwahuwisha wao mpaka kufikia umri ule wangelikipata wapi.

Mhe. Spika, nafikiri sisi Waheshimiwa ambapo katika majimbo yetu kuna uharibifu mkubwa wa mazingira, basi ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba maeneo haya tunayatunza kwa lengo la kuhakikisha kuwa tunakuwa na uhakika wa chakula. *(Makofi)*

Vile vile suala la ukataji ovyo wa mikoko. Mhe. Spika, tulitembelea miongoni mwa maeneo ya Kisiwa cha Pemba kuna eneo kutokana na ukataji miti ovyo wa mikoko bila ya kufuata utaratibu, basi hivi sasa maji ya bahari yamepatiwa njia, yaani bahari imepatiwa njia mpaka kufika katika maeneo ya kilimo. Kwa kweli maeneo ni makubwa ambayo wananchi walikuwa wakilima mpunga na hivi sasa wameingia samaki.

Kwa hivyo, Mhe. Spika hali hii inaonesha dhahiri kwamba hakutomakini katika kusimamia rasilimali hizi za baharini, pia na mikoko kuweza kuizuia ili ardhi yetu isiliwe na bahari.

Kutokana na mwenendo huo ndio unapelekea uhaba wa chakula pamoja na kupelekea wananchi wetu kuwa katika hali ya umasikini wa kipato. Kwa hiyo, wananchi wa kule hivi sasa wanatumia fedha nyingi, yaani karibu shilingi milioni 75 kwa ajili ya ujenzi wa tuta, wakati fedha zile kama lile bonde lao lingekuwa likiendelea kutoa mazao, basi wangeweza kufanya mradi mkubwa wa umwagiliaji maji na kuweza kupata mpunga mwingi.

Lakini matokeo yake kutokana na athari ile ambayo ilifanywa na watu wachache tu, imepelekea kuwepo kwa njaa katika eneo lile na matokeo yake hivi sasa fedha nyingi serikali imetumia, kwa ajili ya kuwapa wananchi wale kujenga tuta, ili kuzuia maji ya bahari yasiingia kwenye mashamba yao.

Mhe. Spika, masuala haya ya uhakika wa chakula kwa kweli yana nyanja nyingi na ni wajibu wetu sisi kama nilivyosema mwanzo tusimuachie Mhe. Waziri peke yake, isipokuwa sisi wenyewe katika maeneo yetu tuhakikishe kuwa kila athari ambayo inayotaka kujitokeza tunaidhibiti. *(Makofi)*

Vile vile kuna huyu adui msumeno wa umeme. Mhe. Spika, msumeno huu ni Juja wa Majuja, maana yake akiingia katika shamba lako basi siku ya pili unaweza ukenda na ukakuta uwanja wa mpira. Sasa uhakika huu wa chakula kama walivyosema wenzangu kwamba kuna mazao ambayo utakuwa unakula wewe mwenyewe, lakini kuna mazao wananchi wanauza kwa ajili ya kupata matumizi mengine na kuweza kufanya shughuli zao nyengine.

Kwa mfano, utakuta miembe, mifenesi, mishelisheli miti hii inachukua muda mrefu sana kuweza kutoa matunda. Kwa hivyo, leo ndugu zetu kwa tamaa yao ya mara moja basi wanakwenda na kuikata miti ile na kuwatia umasikini wananchi wengine ambao wanahitaji kutumia mazao yale kwa chakula.

Mhe. Spika, nilikuwa najaribu kuogelea sana namna ya uharibifu wa mazingira na pia uhifadhi wa maeneo ya vianzio vyetu vya maji. Lakini sina mashaka

sana na mswada huu, isipokuwa kuna eneo moja tu kidogo ndilo limenitia mashaka katika kifungu cha 15 ukurasa wa 107 kwa mswada niliopewa mimi.

Kifungu hiki kinasema kutakuwa na Mkurugenzi ambaye atateuliwa na Rais kwa mujibu wa masharti kama itakavyoainishwa katika hati ya uteuzi. Sasa hapa chini kinachofuata sifa za huyu Mkurugenzi, atakuwa ni mtu mwenye kuheshimika, mwenye sifa na uzoefu katika masuala ya kilimo na uhakika wa chakula na lishe. Sasa mimi hapa sijaona sifa ukiangalia majukumu ya Mkurugenzi itakuwa ni mtendaji mkuu wa Idara atakuwa na wajibu ambao umeeleza, usimamizi wa shughuli za kilimo, usimamizi wa shughuli za kila siku na maelezo mengine chungu nzima.

Siku nyingi hapa tunapopitisha sheria hizi hasa katika ngazi za ukurugenzi mara nyingi waheshimiwa wanashauri basi angalau kuwe na kiwango cha sifa za elimu, kwa sababu ukisema sifa za mkurugenzi awe mtu mwenye kuheshimika heshima ziko za aina nyingi, hapa bado hatujaweka sifa. Sasa hapa mimi naogopa sana pamoja na kwamba Rais ambaye atakuwa na mamlaka ya kutoa nafasi hii lakini vizuri tungelimuwekea na vigezo, kwa sababu wakati mwengine anaweza akaja akateuliwa mkurugenzi pengine atakuwa na sifa za heshima lakini uwezo wa kazi hana hiki chombo ni kikubwa uhakika wa chakula na lishe, basi elimu tunashindwa kuitaja wakati jana tumepitisha hapa mfuko wa elimu.

Sasa kama nafasi nyeti kama hizi kama tutashindwa kuweka vigezo vya kielimu hawa ndugu zetu hamu ya kusoma watakuwa hawana, sasa mimi naomba na kwa bahati mbaya Mhe. Waziri hakuja na tai lakini kama angekuwa kavaa tai mimi ningemng'ang'ania mpaka pakawekwa sifa vyenginevyo tai nitakuwa siiwachi. Mimi nitazuia kifungu hiki tu basi tupate sifa ya elimu tusipeyane kazi hapa kwa kiujomba ujomba. Wakati mwengine huyu Mkurugenzi atakuwa anaongoza watu ambao wana elimu zao watafika pahala watakuja kumdharau, hawa wataalam wetu watakuja kuwa wanatudharau kwa sababu tunawawekea watu ambao kuwa hawana uwezo.

Mhe. Spika, huu mswada ni muhimu sana sasa kutokana na umuhimu wa mswada huu mimi namuomba sana Mhe. Waziri kwa vile ni rafiki yangu sana siwezi hata kumwambia chochote lakini kwa hapa taire, naamini kwamba busara inaweza kutumika ya kumteua mtu huyu lakini naomba kiwango cha elimu kiwekwe hili jukumu ni kubwa sana.

Mhe. Spika, namalizia malizia mwenzangu kazungumzia masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi hili ni suala ambalo sio la masihara, ambalo lazima tuliangalie sasa hivi upepo unakuja bila ya kipimo, mvua zinakuja bila ya viwango. Kwa hivyo hali sasa hivi sio nzuri sana katika nchi zetu.

Lakini vile vile sio mabadiliko ya tabia za nchi tu, mabadiliko ya wakubwa duniani kupigana ovyo sasa hivi unaweza kukaa usiku ukasikia zogo nje ya nyumba ukiuliza nini unaambiwa Rais hatumtaki, sasa kama ingelikuwa zamani mngeliambiwa mnavunja sheria lakini sasa hivi wakubwa wanapelekea kwamba wanaweza kusema hatumtaki rais kwa njia yoyote na wa.o wanaunga mkono, yakuja yakitokezea haya njaa ipo uhakika wa chakula huko kondeni kutakuwa hakwendeki.

Ndio pale inapokuja umuhimu wa kuweka maghala ya hakiba, sasa hivi unaweza kushtukizia wakubwa wanakupiga mabomu tu katika nchi yak ohayo maeneo unayotegemea ya kilimo yanaripuliwa na mambo mengine chungu nzima, kwa hivyo bado upo umuhimu wa serikali yetu kuhakikisha kwamba inakuwa na mahala ya kutoasha kabisa ili janga lolote litakalotokezea basi angalau tulidhibiti, kwa bahati mbaya nchi yetu ni visiwa njaa ikishakutukumba itabidi tukimbilie baharini na ukienda baharini umemalizika kabisa hakuna kama wenzetu kwamba utakwenda kwenye mpaka na kuingia nchi nyengine.

Kwa hivyo, kuna maeneo mbali mbali ambayo yanaweza kusababisha uhaba wa chakula si lazima haya mambo mengine tunayoyazungumza katika uharibifu wa mazingira, lakini hata kuna maeneo ambayo anaweza kuathirika kwa kiasi kikubwa wakashindwa kujitafutia chakula.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa nataka nimwambie Mhe. Waziri mimi nampongeza sana kwa mswada huu, lakini awe hodari sana kuzisisitiza na hizi taasisi nyengine ziweze kuwajibika katika kuhakikisha kwamba huu mswada unatekelezwa kikamilifu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache mimi na wananchi wangu wa Jimbo langu la Kwamtipura tuna asilimia tisini ya kuunga mkono mswada huu, baada ya ile ridhaa ambayo nahisi Mhe. Waziri sio mkaidi sana katika eneo hili la kifungu cha kumi na tano basi nitakamilisha ile asilimia kumi, ili tuhakikishe mswada huu tunautekeleza kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi sina budi kukushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi na mimi kutoa mchango wangu katika suala zima la mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa kujitosheleza kwa chakula MTAKULA namba tatu ya mwaka 1988. Na kutunga sheria ya uhakika ya Chakula na Lishe Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nieleze hapa tulipoanzia kwenye haya maelezo ya mwanzo, katika mswada huu unavyoonyesha ni kwamba tayari

Wizara imejipania kwa sababu inapozungumza kwamba taifa liko tayari kwa sababu ya kujitosheleza kwa chakula, yaani hapa tayari ana uhakika wa kujitosheleza. Lakini la maana mimi nitakalosema kwamba si Wizara tu peke yake lakini sote tufanye kazi moja ya kulisaidia taifa ili kuongeza kiwango cha chakula nchini.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa haki ya chakula tunasema kwamba kila binadamu ni lazima apate chakula, bila ya kupata chakula itakuwa uhai haupo kwa maana hiyo mauti yatakuwa tayari, kwa hivyo ni kitu cha lazima kwa kila binadam apate chakula. Wizara ya Kilimo ndio inatwambia kwamba tunataka tuzalishe chakula kwa wingi, baada ya kuzalisha chakula kwa wingi tutaweza kujitosheleza katika mahitaji yetu ya chakula, si kuzalisha kwa wingi tu lakini chakula chenyewe kiwe cha uhakika na hili uhakika ni kitu cha muhimu sana yaani katika kiwango cha juu, mambo yote yakishawekwa katika uhakika maana yake hayana kasoro.

Lakini tuchukue uzoefu wetu uliopita wa miaka ya nyuma inaonekana katika uzoefu wa miaka ya nyuma katika kilimo chetu chote matatizo ya kimazingira yanatokezea, kwa mfano upungufu wa mvua ni matatizo katika uzalishaji wa chakula, mvua inapokosekana inakuwa ni ukame na ukame huu haumfanyii binadamu tu lakini hata wanyama, hata wadudu wote wanaingia katika ukame sio sisi tu binaadamu lakini hata wanyama wanakosa majani ya kula, wanyama wanakosa na maji ya kunywa.

Kwa hivyo hiki ni kitu ambacho kiko nje ya uwezo wetu hatuna njia ya kusema kwamba tuna uwezo wa kuhakikisha kupata mvua, inawezekana wakati mmoja tukapata mvua na wakati mwengine tukakosa mvua. Sasa lakini tunakuja wakati tunasema tunataka kupigana vita tusikose chakula pasiwe na ukosefu wa chakula ina maana pawe na chakula cha kutosha, hili suala ni zito ni gumu linahitaji mashirikiano ya hali ya juu ili kuweza kuisaidia wizara ili hili lengo ambalo ametupa leo tuweze kufanikiwa. Lakini nataka niseme katika wizara nyingi zilizopo Wizara ya Kilimo ni moja katika wizara ambayo ina wataalam wa kutosha sina shaka katika wataalam, vichwa vipo vizuri ma- *graduate* wengi wapo na wataalam wazuri sina wasi wasi katika hili.

Lakini nasema kuna mapungufu na hakuna zuri lisilokuwa na mapungufu pana mapungufu ya watendaji kazi ambao watu hawa tunataka kuwafikia wakulima huko waliko katika kutoa ushauri. Hapa ndio kwenye matatizo hawana watu wa kutosha kuwapeleka mashambani kwa kuwaelekeza watu katika vipando mbali mbali, sio kipando cha mpunga lakini hata vipando vya mboga mboga, tungule, mabiringani, kunde, mbaazi na kila kitu watu hao wanakosekana.

Hapa sasa nimwambie Mhe. Waziri katika mambo yetu yote tuhakikishe kwamba tunapata watu wa ziada kiutendaji katika maeneo walipo wakulima, hilo ningemuomba Mhe. Waziri atusaidie kwa hilo, hawa tunaowaita mabwana shamba waengezwe ili kufanikisha hilo lengo ambalo tumekusudia.

Lakini jengine Mhe. Spika, sisi tunapozungumzia chakula haina maana kwamba ni ule wali tu, hapa chakula chochote kilichokuwa kigumu, chakula kilichokuwa cha maji maji vyote vikiungana pahala pamoja ni virutubisho vya mwili. Lakini hapa nataka nizungumzie chakula ambacho tunawagawa watu katika makundi. Kuna kundi moja la watoto, kuna kundi jengine la vijana, kuna kundi jengine la wazee na kuna kundi jengine wanawake.

Lakini mimi nashughulika zaidi au nitakuwa na hamu zaidi kutaka kuona suala la chakula nataka nione hali halisi ya watoto, kama tulivyokwishazungumziwa mara ile kwamba watoto wanahitaji lishe mbali ya chakula lakini wanahitaji lishe. Lishe hii kwa watoto ni muhimu sana chakula ambacho atakula mtoto mwenye umri wowote aliokuwa nao kama ni mwaka mmoja, miaka miwili au minne au mitano anahitaji kupata chakula katika mwili wake wa kumfanya huyu mtoto makuzi yake yawe mazuri au akuwe vizuri huyu mtoto. Apate chakula cha kuweza kujenga mifupa yake, apate chakula cha kuweza kufanya harakati zake wakti anapokuwa nje kama mtoto hapati chakula cha kutosha ina maana hawezi kuwa *active* hana harakati zozote. Anakuwa doro na hivyo huyu mtoto anaonyesha ana mapungufu sasa hii Wizara izingatie sana suala la watoto kwamba tunataka tuwape mbali ya hicho chakula lakini lishe bora ambayo itakuwa inawapa watoto nguvu za kutosha.

Makuzi ya mtoto ni muhimu sana kwa sababu ni mtu ambaye tunamtegemea kwa miaka inayokuja kwamba huyu ataweza kutusaidia katika kulijenga taifa hili, tunapoweka watoto ambao makuzi yao yanakuwa mabaya ina maana taifa letu la baadaye la vijana wetu watakuwa makuzi yao ni mabaya.
Mhe. Spika, mengineyo ambayo nasema katika nchi hii uzalishaji tunaelewa hali ya uzalishaji, pia na hapa tuzungumzie katika tabaka lililokuwa muhimu tunataka kuzalisha chakula cha uhakika cha wingi mambo yote yanayohitaji binaadam, mimi nasema pamoja na tathmini tunahitaji kuwa nayo tuangalie katika idadi ya watu ambao tunao katika nchi hii.

Watu wetu ni wangapi ambao wanashiriki katika kilimo kikamilifu tukifanya tathmini tutaona ndani ya nchi hii kuna wazee, ndani ya nchi hii kuna watoto, ndani ya nchi hii kuna vijana, ndani ya nchi hii kuna na wanawake. Tumuulize Mhe. Waziri katika tathmini yake ni nani miongoni mwa hawa niliowataja ambao ni wazalishaji wakubwa, je, wazalishaji wakubwa ni wanawake, wanaume au ni vijana.

Mimi kwa mawazo yangu Mhe. Spika, nasema kwamba asilimia kubwa ya vijana wetu ambao zaidi ya asilimi sitini na tano (65%) ni vijana ukilinganisha katika idadi ya watu basi utakuta vijana hawapo katika mwelekeo wa kuzalisha, hawamo kabisa wao wana habari zao nyengine tu.

Kwa hivyo hapa ningelimuomba Mhe, Waziri wa Kilimo na Maliasili aliangalie kwa macho mawili kwamba vijana wetu wengi ambao ni asilimia kubwa katika suala la uzalishaji wao hawamo hizo habari hawazitaki kabisa, je, Mhe. Waziri hapa utafanya nini kuhakikisha vijana wetu wengi ambao wasopenda kushiriki masuala ya kilimo hatua gani tutawachukulia, vijana wote wanatoka mashamba wanakuja mjini.

Kwa hivyo huu mji umezungurukwa na watu wanaozurura ambao hawana kazi, hawataki kazi na kazi ziko shamba twende tukalime ndio kwenye ardhi. Hapa ningelimuomba Mhe. Waziri ajitahidi kuangalia.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nitalizungumzia ni hii ardhi yenyewe, ardhi ni mali yetu sisi na hii ardhi Mwenyezi Mungu katika visiwa vyetu viwili ameiumba ardhi hii katika tofauti zake, ukiangalia kwa hapa kwetu tulipo Unguja maumbile ya Unguja ni tofauti na maumbile ya Pemba hapa ni tambarare kule ni mabonde na milima. Katika kilimo huwezi kuingiza matrekta kwenye ardhi ya vilima na mabonde hivyo tunaviita vibonde bumbwi uzalishaji wake unakuwa mdogo sana.

Wapi tutapata maeneo ambayo tutaweza kutumia kwa zana za kisasa ni katika ardhi za tambarare ni ardhi nzuri sana kwa kupeleka matrekta yetu.Sasa hapa tunasema ni muhimu Mhe. Waziri akajikaza kweli kweli kuhakikisha kwamba hayo maeneo ya tambarare aweze kupeleka hayo matrekta kwa ajili ya kilimo na uzalishaji mzuri.

Jambo jengine ambalo katika ardhi yetu hii hii tunaiharibu sisi wenyewe binadam, binadamu yoyote naye ni mharibifu sisi wenyewe ni waharibifu hata wanayama baadhi ya wakati wanaambiwa ni waharibifu katika ardhi, unapomfunga mnyama kwenye teremko yamlima ataharibu ardhi ndio maana watu wa Magereza wanachimba misingi na mashimo kuzuia mmong'onyoko wa ardhi, lakini sisi tunaiharibu sisi wenyewe.

Lakini vile vile tunaharibu maumbile ya ardhi yetu Mwenyezi Mungu ametujaalia mito na mito ambayo ni chanzo cha maji tunaondosha miti ile kwenye mito tunaharibu mazingira yapale, ningemuomba Mhe. Waziri katika vianzio vyote vya maji ahakikishe kwamba upo usalama wa kutosha.

Mhe. Spika, kwa hali tunavyoelekea hivi sasa kutokana na *geographical position* ya ulimwengu unavyokwenda kuna mapungufu ya mvua siku hadi siku, ningelimuomba Mhe. Waziri aliangalie sana hili suala. Miongo yetu ambayo tumeiweka minne kwa kuangalia wakati gani mvua zitanyesha sasa hivi ile miongo yetu tuliyoipanga mvua zinakwenda kinyume nyume tukiangalia kama mvua za Vuli au Masika kila mwaka zinaanza kupungua,

Je, Mhe. Waziri unaonaje kama kuna upungufu wa mvua hatuwezi kutumia maji ambayo yapo chini ya ardhi tukawa na maji ya kutosha kuweza kufanya kilimo cha kumwagilia kwenye maeneo ya kilimo huo ni kama ushauri nampa, tusitegemee mvua mara nyingi tukitegemea mvua, hili suala litashindikana utaratibu uwepo wa umwagiliaji hapa tunaweza kufaidika katika suala letu na kilimo kitakuwa kwa wingi.

Mhe. Spika, suala ambalo naliona mimi wenzangu walioanza kuzungumza nyuma mimi nataka kidogo nihitilafiane nalo. Mimi nasema dunia ya leo ni lazima ipatikane *interrelation sheet* huwezi kufanya kitu peke yako, watu wanaofanya biashara wanategemeana huwezi kufanya biashara ukasema mimi kama ni Mzanzibari peke yangu nijitosheleze peke yangu hapana huwezi kufanya hivyo. Lazima uende kwenye nchi nyengine jirani katika ulimwengu na mataifa mbali mbali yale mahusiano mazuri ndio yatakayokusaidia kufanya biashara. Hapa mimi nasema asili ya kusema maneno hayo ni kwamba mwenzangu mmoja aliyezungumza alisema anaweka maeneo sita, lakini katika mawazo yangu nasema zote hizi ziwemo kwa sababu kuna kitu kinaitwa mahusiano huwezi wewe kama ni waziri ukasema nitafanya mambo yote kwa nia hii ni lazima pawe na mashirikiano, mahusiano na kusaidiana baina ya wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, asili ya kusema hili ni kwamba kwa mfano Wizara hii ya Kilimo, Mazingira na Mifugo hapa unatakiwa wanyama wawe wengi, watu wapate chakula cha kutosha na sisi tupate ile *protein* ambayo tunaihitajia, sasa huyo ni lazima awepo. Yeye ndie atakayejua sisi tunahitaji ngombe kiasi gani tuchinje ili *protein* iwepo ya kutosha.

Halafu jengine katika suala zima la uvuvi huko ndiko kwenye *protein* ya kutosha ile lishe yenyewe iko kule ndio pale watu wanaposema watoto wapewe madagaa na vyakula ambavyo vitawasaidia kukuza miili yao, huyu katika wizara hii ni muhimu na hapa ndio tunaondosha ule utapia mko, sasa huyu atakuwemo hana mashaka yoyote katika uvuvi umasikini ataweza kuondosha na utapia mlo utaweza kuondoka.

Halafu katika suala la biashara huyu ndiye dhamana mkubwa hatoki lazima awemo kwa sababu ndio anayetutizamia usalama wa chakula chetu katika

biashara zake, ni lazima atuwekee kwamba chakula hichi ndicho na hichi sicho, hiki kinafaa kuliwa na hiki hakifai kuliwa.

Tukiingia katika watu walioingizwa mimi nasema vijana ni watu muhimu sana haya makundi ya vijana ni lazima tushirikiane nao, hawa ni vijana lazima washiriki katika kilimo na hawa wanalinda makundi yale hatarishi. Kwa hivyo kwa nini tusiwatie vijana hawa ni lazima tuwashirikishe na kwa sababu hawa na vijana wenziwao wanataka waende zao huko mashambani wende wakalime huko, huko kutakuwa na ngazi za kaya na ngazi za taifa.

Halafu katika Tawala za Mikoa ni muhimu sana ambayo tunasema inatoka juu inateremka chini, kutoka juu serikali ambayo inashirikiana na mambo yote halafu inateremka chini hawa ni watendaji hawawezi kutoka wilaya na mikoa lazima waingie, kwa hivyo hapa kwenye vijiji na mashehia yote hawa ndio watakaosaidia katika kuonyesha ile mipango mizima wa huu uzalishaji wa chakula kwa wingi na mahitajio ya wananchi katika wilaya zetu na ufanisi unaweza ukapatikana.

Afya ndio mwenyewe hawazi kutoka kwa sababu huyu tunataka aweze kutathmini hali ya chakula ambacho kinazalishwa ndani ya nchi na yeye ana dhamana ya watu wote, ana dhamana ya wanawake watu wazima na watoto na kila mtu ana dhamana. Kwa hivyo watu wanapokwenda mahospitali huyu ndie anayotoa taarifa kwamba watu wana lishe ndogo, wamekuwa wembamba sana kwa sababu ya udhaifu wa lishe hawana. Sasa huyu moja kwa moja atakuwa yumo.

Halafu katika wizara inayohusiana na maafa hapa mimi nasema ni pahala muhimu kwa sababu maafa ni maafa yanaweza kutokea na wala maafa hayana salama kwamba nitakuja wakati gani, maafa yanaweza kutokezea wakati wowote kuingia katika nchi yetu kama huo ukame, upepo ni maafa, maji lakini sisi alhamdullillahi tuna milima na mabonde kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tunasema kidogo upepo unaweza kutuathiri, wadudu wanaeweza kutuathiri na ukame wa kukosa nguo unaweza kutuathiri. Kwa hivyo hawa wote wanahitaji kukabili hali yoyote ya dharura itakayotokezea ambayo ni ya chakula mpaka ya kifedha, wakati wa dharura ikitokezea watu hawa lazima wasimame mbiele.

Halafu wizara muhimu ambayo ina mahusiano makubwa sana ni Wizara ya Ardhi, Makaazi na Maji na Nishati hatuwezi kulima bila ya maji ni lazima tupate kama ya kisima au maji ya kutoka kwenye mahodhi, maji ni lazima tupate na huyu ataweza kutusaidia katika suala zima la uzalishaji wa chakula chetu. Wizara inayoshughulikia Ardhi nayo ni muhimu kwa vile kuna kitu ambacho yeye ataweza kudhibiti ukataji wa misitu, yeye huyu ndie atakayeona kwamba maeneo makubwa ya tambarare hayana miti akapeleke watu kwa

kusaidiana na wengine ikapandwe miti ili mvua ziweze kupatikana. Kwa sababu kukata miti kwa wingi ni kufukuza mvua.

Mhe. Spika, huyu Waziri wa Fedha na Uchumi ni mtu muhimu sana kwa sababu bila ya fedha mambo hayawezi kwenda huyu lazima tuwe naye bega kwa bega, kwa sababu ni lazima tupate fedha ambazo ndizo zitakazotuwezesha utekelezaji wa sera nzima ya kilimo.

Huyu huyu katika mambo mbali mbali anatupa unafuu wa kodi za wananchi ambazo yeye anazijua kwamba hapa wananchi wanastahiki kupunguziwa na aliwahi kuzungumzia mara moja hapa sisi ndio tunasema bei zikiwa zimekuwa kubwa zaidi yeye ndie anayesema tunapunguza na inapunguzwa kweli. Kwa hivyo watu wote hawa ni muhimu na tunakuwa nao vile vile.

Halafu Mhe. Spika, nasema mambo ya kitaalam ni muhimu katika suala zima hili watu wetu wanahitaji kupewa taaluma ya kutosha kabla suala hili halijatendeka. Wapewe taaluma watu wajue nini dhamira ya serikali katika suala hili kwa sababu lazima papatikane maelewano na mahusiano mbali mbali.

Mhe. Spika, la mwisho ambalo natakakulizungumzia katika mswada huu kuna mambo muhimu, ambalo moja niweze kusema suala la uhifadhi wa chakula *food security*. Hayo ni lazima yapatikane au *food safety* hapa nakusudia kusema ni *food safety policy*, tuwe na sera ya usalama wa chakula. Sasa kama hii haipo *food safety policy* basi ningelimuomba Waziri aiweke tayari hii *food safety policy*.

Jengine Waheshimiwa kuna kitu tunakiita katika vyakula vyetu vyote tunavyozalisha kuna kitu tunakiita *poor food handling* yaani namna ya kuwa navyo vile vitu umeshavipata lakini mtu anaepewa vile vyakula au kitu chochote akashindwa kukihifadhi akaviweka katika hali mbaya ya uchafu, mazingira machafu na ambacho kitu kile anatakiwa mwanadamu akitumie. Hii tunaisema *handling* yake yaani kuwa navyo pamoja pale hali halisi ya matokeo yake ya udhibiti kama huu ni mbovu. Kwa hivyo ningelimuomba Waziri hapa katika *food handling* awe muangalifu sana, kwa sababu hapa tunachunga afya za watu. Kama mambo haya yakitokezea matokeo yake si mazuri mara nyingi huwa ni dayaria. Kwa hivyo mambo yaliyobakia ambayo nimuomba Mhe. Waziri katika suala zima ili tuweze watu wetu kupata mikopo katika Benki hizi.

La mwisho kabisa ingependa kumwambia Mhe. Waziri kwamba hii Wizara ya Kilimo hebu tuweze kulinganisha baina ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Biashara. Wizara ya Biashara watu wengi wanaingia katika Wizara ya Biashara bila ya woga bila ya wasi wasi. Na kwa sababu ya kuingia katika biashara

wanaona katika biashara wanapata faida katika mtandao mzima wa kibiashara. Lakini tunapokuja katika Wizara ya Kilimo tunakuta wawekezaji wanakwenda kuingia katika Wizara ya Kilimo. Tujiulize maswali kwa nini wanakwenda? Kuna lipi ambalo linawafanya wawekezaji wasije kwa wingi kuekeza katika kilimo.

Sasa hapa nimuombe tena Mhe. Waziri alione kwamba hilo wawekezaji hatunao baada, kwa hiyo tutafute mbinu za watu wetu hawa kuingia katika uwekezaji kwa suala zima la kilimo.

Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru na mimi naunga mkono hoja hii mia fil mia. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia fursa hii. Kabla sijaanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) ambaye ametujaalia kukutana jioni hii hapa tukiwa wazima wa afya. Lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kaskazini ambao ndio walioniwezesha nikaweza kufika katika jengo hili.

Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri ambaye ametuletea Mswada huu wa sheria ya kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitoshelezesha na Chakula (MTAKULA) Nam.3 ya mwaka 1988 na kutunga Sheria ya Uhakika wa Chakula na Nilishe Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Waziri kwa kutuletea Mswada huu ambao umetupa mwanga na matumaini makubwa ya kuwa na chakula cha kutosha na kuweza kujiwekea akiba. Mimi kwa upande wangu nimuombe tu Mhe. Waziri kwa kuwa tayari tunajiandaa na hili andalio kusema kweli ni zuri na la uhakika mkubwa kwa sababu mtu bila ya chakula huwezi kuishi. Nimuomba Mhe. Waziri utakapopita Mswada huu na kuwa sheria, basi kwanza kama walivyosema wenzangu tukitaka tufanikiwe zaidi basi ni lazima tuwe na kilimo cha umwagiliaji ambacho kitatufanya sisi tuweze kulima mara tatu kwa mwaka.

Kilimo kile tukiweza kufanikiwa kila miezi mitatu tunaweza tukapata chakula ambacho tunaweza tunavuna mpunga wa kutosha hasa tukizingatia iwapo Mhe. Waziri ataweza kutupatia mbolea, dawa za kuulia wadudu na madawa yanayoulia magugu. Tukifanya hivi tunaweza tukafanikiwa vizuri na ile adhma yetu ambayo ameileta hapa Mhe. Waziri basi tunaweza tukafikia mahala pazuri na lengo likaweza kufikiwa.

Pia nimuombe Mhe. Waziri sheria hii itakapokuwa imekamilika basi ni vyema atuangalie sisi wakulima wa vijiji. Nasema sisi kwa sababu na mimi ni

miongoni mwa wakulima nalima. Niwaombe pia kupitia Baraza hili kuwaomba Waheshimiwa wenzangu ni vizuri tukiwa viongozi tukaweza kuwa kwanza ndio mifano bora ya kuwa tunaweza tukenda tukahamasisha na tunaowahamasisha wakaweza kutuelewa kwa haraka.

Nimuombe Mhe. Waziri kule mashambani kuna watu wanahitaji kulima lakini inawezekana ikawa hawana mashamba. Kupitia Mswada wake huu nimuombe aweze kuweka mkataba maalum ambao utaweza kuwaruhusu wakulima wale ambao hawana mashamba, wale wenye mashamba iwapo itakuwa hawakuyatumia yale mashamba yao, aidha wamepumzika au kwa ugonjwa basi mkataba huu uweze kuwaruhusu wale ambao hawana mashamba waweze kuazimwa mashamba yale waweze kulima kwa wakati ule. Ili ipatikane ile dhana nzima ambayo tunaikusudia ya kuweza kupatikana kwa chakula, mashamba yasikae tu bila ya kulimwa.

Pia nimuombe Mhe. Waziri hasa kupitia hii SEHEMU YA TATU kifungu cha 3 (b) kinachoeleza HAKI YA CHAKULA. Naomba Mheshimiwa ninukuu hichi kifungu ambacho kinasema:

> "uwepo, upatikanaji au uthabiti wa chakula cha kutosha na chenye virutubisho kwa watu wote wa Zanzibar kwa kuweka masharti ya upatikanaji nyenzo za kutosha na zenye kuwezesha, huku ikiweka mazingira mazuri ambayo kaya na watu binafsi wanaweza kufikia na kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora kwa kutumia juhudi zao wenyewe;"

Hapa nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuweka kifungu hichi lakini pia sisi wakulima tunasema juhudi hizi tutakuwa nazo kwa kuwa tunapenda kilimo. Lakini nimuombe Mhe. Waziri au Serikali Kuu inapoweka Bajeti kwa hapa kumesema kutakuwa na nyenzo za kutosha. Nyenzo za kutosha haziwezi zikawepo bila ya kuwa na bajeti ambayo inatosheleza kwa mahitaji. Sasa niombe itakapopitishwa bajeti basi hizi Wizara husika ziweze kupatiwa Bajeti ya kutosha ili ile dhana nzima ambayo tunaikusudia tuweze kuifikia.

Lakini pia kwenye Mswada huu SEHEMU YA NNE kuanzishwa kwa chakula na hifadhi ya chakula Zanzibar. Hii pia Mhe. Spika, niseme nashukuru na nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa katika Wizara yake anao wataalamu wengi, basi itakapofikia wakati huo waweze kutupatia wataalamu ambao wataweza kutusaidia sisi kutufunza katika kuhifadhi chakula. Kwani chakula tunalima sisi wenyewe lakini elimu ya kukihifadhi hatuna. Mfano mdogo tunakuwa tunalima hata mahidi lakini mahindi hayo baada ya kusema tuweze kuyatumia vizuri yaweze kutusaidia kwa wakati mwengine matokeo yake huwa tunayavuna mabichi yote na tukayachoma. Tukanunua mahindi ya kuchoma ambapo hii

tungeliweza mahindi yale yale kuyaanika, tukayakausha na tukaweza kuja kuyatumika kwa wakati mwengine kwa chakula cha kushiba kabisa, ambapo muhimu wa kuchoma ukila huwezi ukashiba.

Mimi nasisitiza, mchango wangu ni mdogo sana. Mwisho nimuombe Mhe. Waziri mpango huu ni mzuri ajitahidi katika utekelezaji na ufatiliaji ili tuweze kuifikia ile dhana ambayo tunaikusudia ya kuwa na chakula kingi cha kutosha na chakula bora au lishe bora.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia juu ya mia ili tuweze kufika katika malengo mazuri ambayo tunayakusudia. Mhe. Waziri nikuombe tu, mipango yetu yote ni mizuri, inataka ufatiliaji na utekelezaji. Kwa maana hiyo tujipange tu vizuri, Ishallah Mwenyezi Mungu atatujaalia tutaweza kufanikiwa na Zanzibar tutaweza kufikia mafanikio mazuri tu.

Mwisho naomba Mheshimiwa maneno siku zote yawe mafupi lakini vitendo viwe virefu. Ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu (SW) aliyetuwezesha jioni hii kukutana katika Baraza lako hili tukufu. Pia sina budi nikushukuru na wewe Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu katika Mswada huu uliyokuwepo mezani.

Sina budi nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyouandaa Mswada huu na kuuleta hapa mezani. Pia nimpongeze tena waziri kwamba baada ya kuuleta hapa mezani hakuuleta tu bali aliufanyia semina na kutupa mafunzo ya kutosha kule *Ocean View* na kwa kweli tulifahamu na tuliuelewa na tulijua dhana nzima ya Mswada huu.
Mhe. Spika, naamini kwamba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wanastahiki pongezi. Kwani nia na lengo la serikali ni kuwapatia wananchi wake chakula cha kutosha tena chenye lishe bora.

Mhe. Spika, taifa lolote lile duniani ambalo watu wake hawana afya basi haliwezi kuleta maendeleo ya kweli, wala haliwezi kuzalisha, wala haliwezi kufika wala haliwezi kujikwamua kiumasikini. Chakula ni msingi wa uhai wa mwanadamu. Katika Semina ambayo Mhe. Waziri alitupatia kule *Ocean View* moja katika mambo ambayo alitufunza ni kujiona sisi wenyewe kwamba bila ya lishe bora hatuwezi kufanya jambo lolote lile wala kuweza kushiriki katika shughuli zozote za uzalishaji.

Mhe. Spika, taifa hili nia na lengo lake kuu ilikuwa ni kuwafikishia wanyonge kuweza kufikia katika hatua hiyo. Naamini kwamba kuwasili kwa Mswada huu mezani na hatimae waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu wakiupitisha, imani yangu kwamba yale malengo na dhamira kuu ya Mswada huu ni kuweza kufanikisha kwa kuweza kujiandaa kwa ajili ya shughuli za uzalishaji.

Mhe. Spika, mimi katika Mswada huu sikuwa na matatizo wala mashaka nao nauunga mkono. Nia ya serikali imegusa hasa pale ambapo pana maumivu makubwa na ndio shida kubwa ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, nchi yoyote duniani inapokosa chakula basi vurugu, zogo na migogoro hutokea. Hivyo basi taifa ambalo halina afya haliwezi kuzalisha, haliwezi kuwa na wataalamu wazuri, haliwezi kuwa na uwezo wa kutoa taaluma yoyote. Mimi katika mswada huu niende kwenye mchango wangu wa ushauri kwa Mhe. Waziri ili tuwe na uhakika wa chakula. Ni lazima Mhe. Waziri afanye tafiti katika maeneo mbali mbali yanayotumika kwa ajili ya kilimo.

Mhe. Spika, wenzangu waliotangulia walianza kusema kwamba Zanzibar ni kisiwa na ardhi yetu ni ndogo. Tukiitumia kiholela bila ya taratibu maalum, bila ya kufanya tafiti kwa kuwatumia wataalamu wetu na kuzitumie zile ardhi ambazo ni tambarare hazilimiki isipokuwa kwa kupata ushauri wa kitaalamu. Namuomba Mhe. Waziri awatumie wataalamu wake kwa kufanya tafiti na hatimaye kutoa taaluma kwa wakulima ili waweze kuzalisha mazao bora, mazuri na mengi kwa sehemu husika.

Mhe. Spika, uhakika wa chakula na lishe haukumalizia kwenye kilimo tu bali pia umeendelea katika sehemu ya uvuvi. Mhe. Waziri atumie au ashirikiane na zile sekta ambazo mwenyewe alizitaja humo katika Mswada wake, katika Sekta ya Uvuvi ili wapatiwe vitendea kazi vinavyofanana na wakati huu vilivyo bora pamoja na taaluma kwa ajili ya kuzalisha samaki hususan na kupata soko.

Mhe. Spika, si hilo tu bali pia chakula na lishe hakimalizii katika utaratibu huo. Mwenyewe Mhe. Waziri ameeleza kwa kina kabisa wale ambao anaamini kwamba wakishirikiana pamoja wanaweza wakafikia hatua cha chakula na lishe. Amewataja na Mhe. Waziri wa mifugo, kwa hakika hawa aliowaunganisha hapa kwa kweli ndio wanaostahiki kabisa kushirikiana nao.
Mhe. Spika, kwenye mifugo kuna hitaji pia kutolewa taaluma. Ardhi yetu tukizingatia ni ndogo tunaihitaji kwa kilimo ardhi hiyo kwa ajili ya mifugo. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba waziri anayehusika anahitaji kutumia ufugaji wa kisasa ulio bora na wa kitaalamu ili tuweze kuzalisha maziwa kwa ajili hiyo ya uhakika wa chakula na lishe kwa Wazanzibari. Pia tuweze kupata nyama kwa

ajili ya kujenga miili yetu na kuitia tija halikadhalika tuweze kuzalisha zaidi kwa ajili ya biashara.

Mhe. Spika, nchi yetu ni kisiwa bila ya kutumia utaalamu hatuwezi kufika. Sisi ardhi yetu ni ndogo tunaihitaji kwa majengo, tunahitaji kwa kilimo na tunahitaji kwa shughuli nyengine za kimaendeleo kama vile viwanda.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awatumie wataalamu tulionao hapa nchini kwa uhakika wawajibike na waweze kufanya kazi katika sehemu walizopangiwa, waachane na ule mwenendo wa kubakia katika maofisi yao. Tabia iliyokuwepo sasa mabwana shamba wote hubakia katika maofisi yao na kule mashambani wakibakia wananchi bila ya kujua ni nani wa kumtegemea.

Mhe. Spika, kwa wakati huu tuliofikia kwa lengo hili la uhakika wa chakula na lishe ni lazima kabisa wataalamu wetu na mabwana shamba wawajibike kuwafuata wadau wetu vijijini kwa ajili ya kutekeleza adhma yetu hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo hii nilikuwa nagusia kuhusu uhakika wa chakula uzalishaji wa ndani. Lakini kutokana na Mswada wa Mhe. Waziri aligusa pia upatikanaji wa chakula kutoka nje akamgusa Mhe. Waziri wa Biashara.

Mhe. Waziri wa Biashara ni lazima awe na uhakika bidhaa zinazoingia nchini ziwe bora na salama kwa ajili ya matumizi ya binaadamu au ya wananchi wetu wa Zanzibar. Mhe. Spika, hatukufanya hilo tu Mhe. Rais wa Zanzibar alichagua mkemia mkuu ili kuweza kusimamia maslahi haya ya Wazanzibar ili waweze kupata afya bora. Ni lazima na yeye awajibike ili isije ikapita danganyadanganya kudhoofisha afya za Wazanziari.

Mhe. Spika, mimi sina mashaka na Mswada huu isipokuwa nina kipengele kimoja hapa naomba Mhe. Waziri atakaporudi tena kufanya majumuisho yake basi naomba anipatie maelezo kidogo. hiki ni kifungu cha 20(4) kinasema hivi:-

> "Endapo mtu ametambuliwa kuwa katika Mazingira hatarishi chini ya Sheria hii na anakosa au yupo katika hatari ya kukosa chakula cha kutosha au utapiamlo Serikali itampatia mtu huyo kiwango cha chini cha chakula."

Mhe. Spika, hapa sikumuelewa kidogo Mhe. Waziri naomba anipe ufafanuzi maana akisema chakula cha kiwango cha chini nashindwa kumuelewa. Hivyo Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifafanulie hili ili niweze kufahamu. Dhamira yetu ya uhakika wa chakula ni kupata chakula kingi na cha kutosha. Lakini anasema mtu huyu atapata kiwango cha chini mtu

huyu ambaye ameishiwa. Na sisi tumesema mpango huu unawahusu Wazanzibari wote bila ya kubagua rangi, dini wala kutumia usiasa ndani yake. Hivyo basi namuomba Mhe. Waziri aniweke vizuri hapa.
Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono Mswada huu kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kaskazini (B) Unguja. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii leo kuweza kuchangia Mswada huu ambao umetayarishwa na Mhe. Waziri wa Kilimo.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na sote humu ndani wajumbe wako Baraza kuwa na pumzi ya kuweza kuchangia Mswada huu kwa makini kabisa.

Mhe. Spika, namshukuru sana Waziri pamoja na Katibu wake, Naibu Katibu, Wakurugenzi pamoja na maafisa wake kwa kukaa kwa utulivu kabisa na kuweza kutuleta sheria hii ambao wao wameona kuwa Zanzibar sasa hivi inahitaji lishe. Lakini katika hali hiyo walituona katika asilimia ambayo kubwa inatudhoofisha kutokana na ukosefu wa kupata lishe na ndio maana wakaamua kutuletea Mswada huu na sisi wajumbe kuweza kuuchangia.

Mhe. Spika, mimi nitaanza kwa jumla jumla halafu baadaye nitaingia kwa ridhaa yako nitaingia katika vifungu ambavyo nimeviona vina kasoro ili Mhe. Waziri baadaye ataweza kunisaidia kuvirekebisha. Lakini katika hayo ya jumla jumla kuna *point* ambazo ndani yake Mhe. Waziri ataweza kuzipata.

Mhe. Spika, kwa kweli Mswada huu umekuja wakati mbaya sana na hili tukiri. Kwa sababu lengo hasa la Mswada huu tuwe na maeneo. Lakini maeneo sasa hivi hayapo, huo ukweli tuseme, maeneo yote tumeyachukua viongozi, utakuta kila kiongozi ana heka tisa tisa. Kweli mheshimiwa dhamiri ya lengo hili litakuwa. Kwa sababu ya kutokuwa na lishe wananchi wa Zanzibar, msaada mkubwa sana unachangia kutokana na vyakula ambavyo vinatoka nje vinakuwa vina sumu, sasa hata muda ile sumu ya kuweza kukaa kwenye ghala ya nje mpaka vinafika Zanzibar kwa kweli tayari inamu-*effect* mtu vile virutubisho vya ndani ya mwili wake binaadamu vinakuwa vinakufa kabisa, hatimaye anakosa lishe kutokana na hali hiyo.

Mswada huo maelekezo yake kuwa lengo kubwa ni asilimia kubwa tujitosheleze wenyewe katika ardhi yetu. Tutakapokuwa tunalima mboga mboga, mipunga, vile vitakuwa vipo safi kabisa kwa mtu anaweza akala na akapata lishe ambayo iliyo ya uhakika inayotakiwa. Ndio maana nikasema nasikitika kabisa kuwa maeneo sasa hivi hakuna ya wakulima tukubaliane hivyo.

Mhe. Hamza alisema kuwa wengine wamefanya makaazi, wengine ndio hivyo kama tunavyosema wamejikumbia wao wenyewe bila ya kuona wananchi jinsi gani ambavyo wataweza kuwasaidia.

Mhe. Spika, niende kwenye suala la umwagiliaji wa mpunga. Kwa kweli hatukuwa na umeme wa uhakika Zanzibar. Suala hili la umeme Zanzibar unapunguzia mambo mengi, hata hiyo lishe yenyewe hatuipati. Siku zote tunasema jamani tuwe na umeme wetu mbadala. Kwa kutegemea jamani kibatari cha jirani kila siku tutafika pahali tutakuwa giza. Sasa leo kuna mambo mengi Mhe. Waziri anataka kutuandalia kutuletea njia ambazo binaadamu aweze kulima tusitegemee ulimaji wetu kila siku wa mvua.

Mheshimiwa mvua sasa hivi kama tunavyojua inakimbia. Inakimbia kwa sababu vianzio vya mvua tunaviondosha kabisa. Wenzangu wengi wamekimbilia katika masuala ya mazingira. Masuala ya mazingira mimi siwalaumu wadogo nawalaumu wakubwa ndio tunaochangia kwa asilimia kubwa. Mkoa wa Kaskazini tunaoharibu ni sisi viongozi. Mazingira ya Mkoa wa Kaskazini ni mabaya sana, hata ile ardhi ukiambiwa leo uende ukalime unashindwa kuipata kwa sababu imechimbwa mchanga na ile rutba ya chini unaikosa kabisa au kwa jina jengine kile kimea cha chini ambacho kitaweza kukusaidia wewe rutba ya ardhi ili uweze kupata chakula kizuri basi inakosekana katika ardhi zetu.

Mhe. Spika, nilisema siku moja kuwa utaratibu na Mhe. Waziri mwenyewe yupo naendelea kumwambia. Suala hili Mheshimiwa bado linaathiri kabisa, kama sheria haikufuata mkondo wake basi tutaendelea kuharibikiwa kabisa katika maeneo ya Kaskazini Unguja. Tusijisifu kuwa tutakuwa na kilimo kingi, si kweli. Tuseme ukweli na uwazi.

Mheshimiwa muhusika wa mazingira bado kwa Kaskazini hali inaendelea minazi inaangushwa kwa kuchimbwa mchanga, miembe inapotea, mfuu sasa hivi Kaskazini hakuna umeshakwenda na maji kwa sababu umeshachimbwa mchanga. Mheshimiwa utaratibu huu wa kuchimbwa mchanga tusiwaachie watu wa Halmashauri, waachieni wenyewe watu wa misitu ndio wanaojua utaratibu ulivyo, wana utaratibu mzuri kabisa lakini kwa tamaa yetu tunakwenda kuwapa watu wa Halmashauri, hatimae ardhi inapotea. Tamaa tu hakuna kitu chengine chochote, hazitutoshi fedha sisi wakubwa, hazitutoshi fedha tunazolipwa kwenye mishahara, tunathamini hii kazi nyengine. Hili ni lazima nilikamatie uskani dhahiri kwa sababu hali ngumu sasa hivi ardhi inateketea.

Mheshimiwa juzi tu niseme kule sehemu ya Fuoni wachimbaji hawa kiholela wa mashimo kuna mtoto wa miaka 13 ameona ende akakoge basi kenda akanasa na akafa hapo hapo kwa sababu kunachimbwa michanga ni hatari na kipindi kama hiki cha mvua. Kwa hivyo, hili naomba tuliwekee mazingira mazuri Mhe. Waziri nakuomba kwamba uliweke kwenye mkakati mzuri ili kuweza kufanikisha jambo hili.

Mhe. Spika, tukija katika suala la vijana kusema kwamba hawapendi ukulima ni kwamba mimi nakata, ni kwamba wanapenda lakini ni kuwa vitendea kazi hawapewi. Kwa mfano, Upenja pale nenda katizame vijana wanalipa kilimo cha kisasa vitu mbali mbali hivyo wizara yako imeshawaomba wapate angalau zile bomba za maji ili yaweze kuwasaidia katika kazi zao za kilimo. Mhe. Spika, ni kwamba ukweli tuuseme vijana hao wamepiga kelele mpaka wamechoka na wengine hatimae wanapata matatizo kwa kupanda ngazi na kushuka na mpaka leo hakuna walichoambukia. Kwa hivyo, dhana hii ya kuweka mswada huu kama hatukuwa makini katika hali hiyo basi tusidanganyane mimi siku zote nasema kilicho wazi.

Mhe. Spika, ni kwamba tukipanga kitu tuwe na usimamizi mzuri kwa sababu tunaangalia athari ya wale watu wetu lakini baadae tunaidharau. Kwa hivyo, hili hakuna kijana asiyependa kulima hata siku moja, vijana wanajishughulisha vizuri, ardhi hiyo hiyo ndogo waliyopata lakini wanaiboresha vizuri lakini hatimae zana zenyewe za kufanyia kazi zinakuwa hamuna.

Mhe. Spika, kule Dar es Salaam kila siku mimi huangalia televisheni utakuta wenzetu wanapewa vitu vya kisasa kabisa mtu anafurahi kabisa kushughulikia shamba lake. Lakini sisi leo tunatoka na majembe hivyo lishe itapatikana wapi au sisi wenyewe tunakaa hapa tunapiga makofi na bajeti ya watu wa kilimo tunawapa kidogo, hivyo kweli wizara itaweza kufanya mambo mazuri. Mhe. Spika, mara hii tutaisaidia kabisa Wizara ya Kilimo ili tuone katika bajeti yake inapita mia juu ya mia na tuone katika bajeti yake inapita mia juu ya mia na tuone maendeleo yake.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kuwa umeme wetu sasa hivi ni hafifu na hivi sasa tuna umeme wa mgao, hii ni hatari moja kubwa. Mhe. Spika, umeme huu wa mgao kuna mambo mengi mheshimiwa yatatupungukia na hasa kama nilivyosema kuwa hatukuwa na tahadhari.

Mhe. Spika, wenzetu sasa hivi kule Bara kila siku zikenda wanatafuta mbinu, juzi nimeangalia televisheni wana mbinu sasa hivi ya kutafuta umeme wa upepo. Mhe. Spika, sisi mpaka leo Zanzibar tumekaa tunangojea kaka tuwashie umeme, jamani hatuoni kama hii ni hatari hivyo tunaogopa nini, kwa nini na sisi tusitafute mbadala wetu, kule Makunduchi kuna mawimbi tele tunaweza

tukafanya umeme lakini mpaka leo sijui ni kwamba tunaogopa, mimi naona sielewi ni sababu gani inayotufanya tusitafute miundombinu ya kupata umeme uliokuwa wa uhakika. Mhe. Spika, sasa hivi kuna miundombinu ya rahisi tu na bei inakuwa ni ndogo umeme wa gesi, hilo nalo hebu tuliangalie kwa makini.

Mhe. Spika, sasa hivi naingia katika mswada wenyewe. Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 101 katika kifungu cha 3 kijifungu kidogo (2) inasema sheria hii itasimamia masuala yote yanahusiana na uwepo wa chakula. Mhe. Spika, hapa kidogo kuna kitu kimeruka hapa au vipi namuomba Mhe. Waziri sentensi yako iwe nzuri utakuja kuniambia hapa una kitu gani ambacho kitaweza kifahamike "uwepo" au "kuwepo".

Mhe. Spika, pia kifungu cha chini hapa kuna chakula maana yake ni kirutubisho kinachokubaliana kikiwa katika hali ya ugumu wa maji maji. Mhe. Spika, tafsiri siku hizi ziko nyingi za Kiswahili kwa hivyo ningeomba kidogo nahili nalo linanisumbua. Kwa sababu naelewa wazi kuwa mwili haujengwi na zege, mwili unajengwa na virutubisho lakini hapa umeniambia kuwa vigumu, ni nini kigumu kinanisumbua hapa mheshimiwa. Kwa sababu naamini kwamba *concrete* haiwezi kuingia ndani ya tumbo, ni moja katika ishara ya ugumu. Lakini sasa hapa mimi nafahamu ugumu unanishughulisha hapa nakuomba Mhe. Waziri unisaidie ili niweze kufahamu kabisa.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 102 hapa msaada wa chakula maana yake ni chakula kilichotolewa kwa njia ya mswada na mtu aliyebainishwa kuwa na hali hatarishi kwa mujibu wa sheria hii. Mhe. Spika, kifungu hiki mimi bado sijakifahamu hali hatarishi hii vipi, huyu mtu ametuletea chakula kibaya ndio tunapewa taarifa mapema. Mhe. Spika, hili mimi nakaa mbali kweli hiki Kiswahili kimenipa tabu sana niseme ukweli wangu hivyo, ningekuomba na hili nalo uweze kutusaidia ili niweze kuunga mkono vizuri sana.

Mhe. Spika, ni kuhusu suala la msitu ni kwamba msitu wa Kiwengwa unateketea, Zanzibar hii imebakia misitu miwili tu kwa historia na Pemba ni mmoja tu. Kwa hivyo, mheshimiwa tusipoujengea mazingira mazuri kuna viongozi wengine wanapiga kofi umalizike, viongozi wengine tunaumia ndani ya nafsi. Nini maana ya kusema hivyo? Kiongozi mmoja akikamata wananchi waliokata msitu, basi kiongozi mmoja anakwenda kuwatoa. Kitu hiki kinasikitisha kweli tena hivyo sisi tunakwenda wapi. Mhe. Spika, nasema tusiogope kunyimwa kura kuliko kuukosa msitu, katika msitu ule mna vyanzo vya maji ambavyo vinasaidia wananchi pamoja na wageni wanaokuja. Lakini kwa mazingira hayo utakuta kiongozi akudhalilisha kusema ukweli Mhe. Waziri hili uliangalie vizuri sana tunadhalilika viongozi tunaoshughulishwa na misitu hiyo.

Mhe. Spika, ni kwamba huu ni wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hakuna pahali pa kuogopana ni kuwa tuambizane ukweli. Kwa hivyo, mimi naomba sheria kama imelegeza basi ikazwe kamba ili tuukamate msitu wetu wa Kiwengwa kwani unateketea tuuzuie ili watu wasiuteketeze. Mhe. Spika, nawashukuru wananchi wangu wa Kiwengwa ni walinzi wazuri sana na jengine la kusikitisha hata hivi vikosi vyetu vya serikali vinakwenda kukata miti kule. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri nalo hili tuliangalie na wale wanaouzunguka ule msitu watafutiwe nyezo nyengine za kufanya ili waondokane na ukataji wa kuni wende katika teknolojia ya kisasa za sasa hivi. Kwa hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope mia kwa mia.

Mhe. Shawana Bukheti Hassan: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kuweza kusimama tena kwenye Baraza hili lako tukufu kuweza kuwakilisha wananchi wa Jimbo la Dole. La pili nikushukuru na wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii japo ya mwisho mwisho lakini nitajitahidi kuyasema yale ambayo nimeyakusudia kwa hii leo.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana ndugu yangu Mhe. Mansour Yussuf Himid (Waziri wa Kilimo na Maliasili) kwa nia yake nzuri yakuteletea mswada huu ambao ni mswada mzuri na unatia matumaini kwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, suala la chakula ni suala muhimu sana kwa nchi yetu na wajumbe wote nadhani wamelizungumza hilo na mimi nakubaliana na wao bila ya chakula cha uhakika na bila ya kuwa na chakula ambacho tumekihifadhi kwa kweli inawezekana ikawa ni tatizo.

Mhe. Spika, sasa hivi katika nchi yetu yanaweza yakatokea yoyote na kwanza inaweza ukatokea ukame, mwenzangu hapa ameeleza suala la ukame halitabiriki na kama hatuna chakula cha uhakika kwa kweli ni tatizo. Kwa hivyo, nampongeza sana kwa hili watu wamesema penye nia pana njia pamoja na mambo mengi yaliyoelezwa, mapungufu mengi yaliyoelezwa lakini nina imani kama tutaungana pamoja basi tutafanikiwa.

Mhe. Spika, jengine katika suala zima la hali ya kidunia sasa hivi ilivyo, tumeweza kusikia kwenye vyombo vya habari na vyengine tumeona katika hali nzima ya dunia ilivyo mambo ya vita yanavyoendelea. Bidhaa zinavyopanda bei na wakati mwengine bidhaa zinakuwa tayari zinataka kusafirishwa pamoja na chakula kuja katika nchi zetu lakini utakuta kuna maharamia humu katika mabahari vyakula wanaviteka nyara. Lakini tutakapokuwa na uhakika wa chakula katika nchi yetu mambo mengi haya yatakayotokea kwa sisi yatatupa nafuu. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa hili na naamini hali itakuwa nzuri.

Mhe. Spika, katika masuala ya chakula tumeambiwa ni suala la chakula na lishe. Mhe. Suleiman hapa kidogo amenifilisi kwa sababu chakula ni chakula tu cha jumla, lakini unaposema lishe pia ni chakula ambacho kinatakikana mwanadamu aweze kukipata. Mhe. Spika, chakula kimegawika katika maeneo nadhani kama matatu. Chakula tunasema kuna *protein*, kuna *vitamin* na kuna *carbohydrate*. Kwa hivyo, mwanadamu haya yote anatakikana ayapate, kimtazamo wangu mimi nilivyoona katika upatikanaji huu wa chakula nimeona tunaweza tukajikita sana katika chakula hiki cha *carbohydrate* labda kama mchele, muhogo na mambo mengine. Lakini katika *protein* sijui kama tumejipanga vizuri katika suala hili na kama hatujajipanga vizuri basi mimi ningemuomba Mhe. Waziri yale waliyoyazungumza wajumbe katika masuala mazima ya *protein* kuweza kupata samaki na mambo mengine yote nayo yachukuliwe kipaumbele kuona tutafanyaje ili hawa wananchi wetu waweze kufaidika kupata chakula na lishe.

Mhe. Spika, jengine katika chakula kama nilivyosema mna vitamin, na vitamins hasa tunazosema hapa mara nyingi tunatumia pia vitamin C na hii inatokana kwenye matunda. Kwa hivyo, sijui Mhe. Waziri katika hili la chakula na lishe suala hili la matunda sijui tuna utaratibu gani wa kuweza kulihifadhi. Mhe. Spika, kuwa utapata chakula lakini hapo hapo chakula hicho tuweze kukihifadhi, lakini sijui utaratibu wizara imejipanga vipi katika kuhifadhi matunda. Maana yake matunda ni masuala ya msimu yanaweza yakawepo leo na kesho hayapo na wakati mwengine yanakuwepo kwa wingi lakini kwa vile utaratibu wetu wa kuyahifadhi sio mzuri hivyo baada ya muda matunda hayo yanakuwa hayaharibika. Kwa hivyo, angetusaidia Mhe. Waziri juu ya haya matunda tutayahifadhi vipi.

Mhe. Spika, masuala mengine mengi yameshazungumzwa katika kupatiwa elimu watu wetu. Kwa kweli Mhe. Spika, suala la elimu kwa watu wetu bado halijawafikia hasa vya kutosha. Hasa katika masuala haya ya kulima mboga mboga, matunda na kadhalika. Mhe. Spika, kuna msemaji mmoja hapa alizungumza suala zima la hawa wataalamu kuwa wanabaki maofisini. Kwa kweli Mhe. Spika, katika wizara ambayo ina wataalamu wengi ni Wizara hii ya Kilimo, lakini utakuta maeneo mengi wataalamu hao hawaonekani, na wananchi wetu wanahitaji utaalamu wa kuelimishwa.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana hao wataalamu wake wajitahidi kusomesha sana, mimi katika jimbo langu ninacho Chuo cha Kilimo pale wanafundisha mambo ya kilimo. Lakini wakishamaliza masomo wataalamu hao hatuwaoni kwenye mabonde kuna watu wengi sana wanahitaji utaalamu huo katika masuala ya kupata elimu. Kwa hivyo, ningemuomba sana

Mhe. Waziri hao wataalamu wake wateremke kwenye mabonde ili waweze kutusaidia.

Mhe. Spika, katika mswada huu kuna afisa mmoja ameambiwa kila Wilaya apatikane afisa mmoja. Mimi nitaungana pia na hili kuna msemaji mmoja yeye alisema ni Mkurugenzi lakini mimi nimeangalia kwenye afisa, maafisa hawa watakaoteuliwa hatukuona vigezo vyao ni nini au elimu yao iwe vipi au watakuwa ni maafisa tu maana yake hili suala linahitaji utaalamu ndani yake. Mhe. Spika, chakula na lishe lazima liwe na utaalamu huwezi mtu yeyote tu ukamchagua au ukamteua akawa hana utaalamu akaweza kuifanya shughuli hii.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka nimalizie humu ndani ya mswada wenyewe kwenye madhumuni katika vipengele vilivyokuwa vinaoneshwa vya sehemu mbali mbali nimehisi haviendani sambamba na ndani ya mswada wenyewe. Kwa mfano, sehemu ya tatu unaweza ukakuta suala la masharti juu ya maelekezo, lakini ukija kusoma kwenye mswada utakuta kumeandikwa jawabu nyengine. Pia Mhe. Spika, sehemu ya nne inayohusu haki ya kupatikana chakula, lakini sehemu hii kwenye mswada wenyewe utakuta ni sehemu ya tatu na halafu pia katika mswada huu huu utakuta kuna sehemu ya tano na ya sita, lakini huku kwenye vipengele unakuta sehemu ya sita na ya sita na maana zake nazo ziko tofauti.

Kwa hivyo, mimi ningeona Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho hebu huu mswada uwe unajipanga vizuri, hii sehemu ya tatu ijuulikane hasa kama ilivyo, na nne ijulikane kama ilivyo na ya tano ambayo haimo humu kwenye mswada inaonekana haimo lakini huku unaikuta kuna ya sita na sita, na sita pia ina maana tofauti na kipengele hiki kilichomo humu. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho basi na hili aliweke sawa. Najua Mhe. Spika, muda ulionipa ni mbaya sana kwa nilivyojipanga inabidi nizungumze haraka haraka lakini na mimi ilimradi japo mawili matatu nimeyazungumza. Mhe. Spika, kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Dole naunga mkono mswada huu asilimia kwa mia.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Shawana Mhe. Waziri amekusikia na amefahamu. Waheshimiwa Wajumbe kuna matangazo mawili kuhusiana na semina zetu za kesho, semina ile inayohusu mswada wetu wa haki ya mtoto itafanyika Zanzibar Beach Resort badala ya hapa saa ni zile zile, semina itaanza saa 3:00. Hivyo, tunaombwa katika semina hiyo tusisahamu kuchukua ule mswada unaohusu haki ya mtoto ili iwe ni rahisi kufanya marejeo katika taaluma tutakayopewa pale.

Sehemu ya pili ni semina kuhusu rasimu ya kukabiliana na maafa, semina hii itakuwepo hapa hapa Barazani saa 8:30 mchana mara baada ya kumaliza semina ya kule mnamo saa nane mchana. Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa umeme umetukatalia naahirisha kikao hiki hadi tarehe 28/03/2011 siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi saa 3:00 asubuhi ya tarehe 28/08/2011)